

**KANE AKERWA NYOTA KUIKACHA ENGLAND**
UKURASA 22

**FURSA** kwa Tanzania Mkutano Mkuu G20
UKURASA 3

**MBARONI** madai ya kumuua bibi, kisha kukata titi na sehemu za siri
UKURASA 5

**MABEHEWA** 260 mizigo reli ya SGR kuwasili mwezi ujao
UKURASA 8

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumamosi Novemba 16, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581862
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
LIKE & FOLLOW US 0745 700 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Serikali yasema jambo usawa kikokotoo mafao

**YASEMA** suala la uwiano watumishi serikali, sekta binafsi linazungumzika...
*Endelea ukurasa wa 3*



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete

Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya

## TEC yatoa tamko zito kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa
UKURASA 2



RIPOTI MAALUM

## Ukame ulivyobadili asili jamii Wamasai
UKURASA 4




Skani hapa kutembelea chaneli yetu

MICHEZO GAMONDI YAMETIMIA, APIGWA FAINI UK. 24 KATUNI UK. 6

# Mradi umeme Rusumo wafikia asilimia 99.9

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Mawaziri wa Nishati wanaosimamia Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo ambao wanatoka nchi za Tanzania, Burundi na Rwanda wamekutana na kujadiliana kuhusu mradi ambao utazinduliwa karibuni.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambaye pia ni Mwenyekiti wa baraza hilo, Dk. Doto Biteko alisema jana kuwa pamoja na mambo mengine wamekubaliana mawaziri warejeshe makubaliano yaliyofikiwa na kikao kwa marais ili waridhie uzinduzi rasmi.

"Mradi umefikia asilimia 99.9 na vimebaki vitu vichache ili kuukamikisha, katika kikao cha Baraza la Mawaziri kuhusu mradi tumekubaliana kuwasilisha maombi yetu kwa wakuu wa nchi ili watakapopata nafasi mwakani, wazindue mradi huu," amesema Dkt. Biteko.

Alisema sasa mahitaji ya umeme Tanzania ni Megawati 1,800 na ina uwezo wa kuzalisha Megawati 3,070, hivyo kuna ziada ya umeme.

"Kuwa na vyanzo vingi ya umeme maana yake tunakuza uchumi wa nchi yetu. Asilimia 52 ya umeme wote tunaozalisha unatumiwa na wananchi na asilimia 48 unatumika kwenye viwanda," alisema.

Dk. Biteko alitaja manufaa ya mradi huo kuwa hadi sasa umezalisha ajira kwa watu pamoja na kusaidia uwepo wa miradi mbalimbali kwa ajili ya huduma kwa jamii husussan katika Halmashauri ya Ngara (CSR).


Aidha, mradi huo umeiunganisha Tanzania, Rwanda na Burundi na pia unatoa fursa ya kuziuzia umeme nchi hizo endapo zitahitaji licha ya megawati 27 zinazopatikana kwa kila nchi.

Katika hatua nyingine, Dk. Biteko alioa rai ya utunzaji wa mradi huo ili uendelee kutoa umeme.

"Mradi huu hauwezi kuwa wa kudumu kama hatutunzi mazingira na leo (jana) tumetoa maelekezo kwa Baraza tuanze kupanda miti katika eneo la mradi ili kuendelea kutunza mazingira na kuwa na vyanzo vya uhakika vya umeme," alisema.

Mradi huo umeanza kuzalisha megawati 80 ambazo zinagawanywa kwa usawa wa megawati 27 kwa Tanzania, Rwanda na Burundi, hivyo kuzidi kuimarisha gridi za taifa za umeme.

Mradi huo unaotekelezwa na Kampuni ya Umeme ya Rusumo (RPCL) inayomilikiwa na nchi zote tatu, ni kielelezo cha azma ya serikali ya Tanzania kuhakikisha kunakuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika kwa ajili ya shughuli za maendeleo na kijamii.



Rais wa Zanzibar, Alhajj Dk. Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Mtoto, Hassan Saleh alipowasili katika Msikiti wa Maungani kwa Hafidh Ali, Wilaya ya Magharibi "B" Unguja jana, kujumuika na Waumini wa Dini ya Kiislam katika Ibada ya Swala ya Ijumaa. **PICHA: IKULU**

# TEC yatoa tamko Uchaguzi Serikali za Mitaa

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC) limesisitiza kuwapo na mfumo wa wazi, haki na unaowajibika katika kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Rais wa TEC, Askofu Wolfgang Pisa, alisema kuna madhara makubwa ya kukosekana kwa uchaguzi wa haki ikiwamo malalamiko kutoka kwa wananchi na wakati mwingine nchi kuingia katika vurugu.

"Sisi TEC tusingependa nchi yetu itumbukie katika vurugu zinazosababishwa na uchaguzi mbovu. Njia ya uhakika na ya kuaminika ya kuepuka suala hilo ni kupata viongozi kwa kuendesha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa njia ya haki, uhuru, uwazi, utu, demokrasia na upendo," alisema.

Askofu Pisa alisema wananchi wameshuhudia namna uandikishwaji wa daftari la makazi ulivyofanyika kwa njia zisizo na haki ikiwamo kutokutolewa kwa vitambulisho vya wapiga kura na kuenguliwa kwa wagombea wengi kutoka vyama vya upinzani jambo liliioitia serikali doa.

"Na hata pale kiongozi mwenye dhamana alipoamua kutoa muda zaidi wa kukata rufani bado hakuondoa doa hilo kwa uchaguzi wa mwaka huu," alisema.

Alisema ili kuhakikisha wananchi wanaitumia vizuri haki yao ya kuanzisha na kuendesha serikali ya mitaa ni lazima kuwe na mfumo wa wazi, wa haki na unaowajibika katika kusimamia mchakato wa uchaguzi wa viongozi kuanzia ngazi za chini.

Aliikumbusha serikali kutambua nafasi yake katika uchaguzi huo ya kuwawezesha wananchi katika mitaa, vitongoji na vijiji ili kuwapata viongozi halali watakaowawakilisha na wale wataoshinda kihalali ndio wanaopaswa kutangazwa.

Askofu Pisa alisema ni muhimu katika ngazi ya serikali ya mitaa kupatikana viongozi waadilifu na waaminifu, kwani ndiko sehemu ambayo raia hupata fursa ya kutathmini utendaji, uwajibikaji na uwazi wa serikali katika kutekeleza majukumu yake kuanzia ngazi ya mtaa hadi taifa.

Alisema kiongozi anapochaguliwa kwa kupitia ulaghai, hata uongozi wake unakuwa sio wa kiadilifu, kwani atawaongoza watu kwa kutumia nguvu katika kipindi chote cha uongozi wake.

"Na viongozi wa namna hiyo wakati mwingine tusishangae hata baada ya kuchaguliwa wasipofika kwa watu kwa sababu wanaona hawana dhamana ya kuwaongoza watu husika," alisema.

Rais huyo wa TEC alisema taifa linapaswa kulelewa na kufanya kazi katika ukweli na si kutengeneza jamii yenye ulaghai, kwani Mungu hadanganyiki wala hadanganyi na angependa sasa watu wake waendelee kuishi katika misingi ya haki na ukweli.

Alisema tunapoelekea katika uchaguzi huo hawana budi kama viongozi wa Kanisa Katoliki na kiroho kuungana na Watanzania katika upatikanaji wa viongozi kupitia uchaguzi huru na wa haki .

"Kanisa Katolini huthamini na kuenzi namna Watanzania wanavyoshikamana na kutamani kujitawala, rejea Warumi sura ya 13 mstari wa kwanza hadi wa saba," alisema.

Aliwasihi wananchi wajitokeze kwa wingi katika kupiga kura za kuwachagua viongozi katika ngazi hizo kama walivyotangaziwa na kuiomba serikali kuhakikisha kuwa demokrasia inatawala nchini na kutuma ujumbe kwa dunia.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# MNH-Mloganzila yazindua kitengo unyonyeshaji njiti

**Na Christina Mwakangale**

HOSPITALI ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, jana ilizindua Kitengo cha Kuhifadhi na Kuratibu Maziwa ya Mama kuhakikisha watoto njiti wanapata maziwa ya mama zao kwa wakati.

Aidha, wataalam wa afya nchini wamesisitiza kuendelea kuwa mstari wa mbele katika kupigania maisha ya watoto wachanga wanaozaliwa kabla ya muda, ili kupunguza vifo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi, alisema hayo jana wakati akifungua maadhimisho ya kuelekea siku ya mtoto aliyezaliwa kabla ya muda (njiti) yaliyofanyika katika MNH-Mloganzila.

Alisema lengo ni kufikia mkakati uliowekwa ifikapo mwaka 2030, vifo vya watoto wachanga kuwa chini ya vifo 12 katika kila vizazi hai 1,000 .

Prof. Janabi alisema kila watoto 1,000 kuna watoto wachanga wapatao 24 wanaofariki dunia ndani ya siku 28 za kwanza na kwamba mikakati ya kupunguza vifo hivyo haiwezi kuwa endelevu bila kushirikiana wadau katika sekta ya afya na kuboresha ujuzi wa kuhudumia watoto hao.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya, imekuwa ikiratibu progamu mbalimbali ambazo lengo lake ni kupunguza vifo vya watoto wachanga na walio chini ya miaka mitano, programu hizo ni kama kumsaidia mtoto kupumua baada ya kuzaliwa, kupanua huduma za watoto wachanga kwa kujenga wodi za watoto wachanga hospitali za mikoa na wilaya na kutoa mafunzo kwa wahudumu wa afya ya namna ya kuhudumia watoto wachanga.

Bingwa Bobezi wa Watoto Wachanga MNH, Dk. Martha Mkony, alisema katika Afrika takribani mtoto mmoja kati ya 10, huzaliwa kabla ya wakati na watoto hao hukabiliwa na matatizo mbalimbali kama vile kupumua, maambukizi na hatari za ukuaji kwa muda mrefu.

"Pamoja na kuwapo kwa changmoto hizo, lakini bado kuna matumaini kupitia juhudi za serikali, kwani kuna maboresho ya kutia moyo katika utunzaji wa watoto wachanga nchini kwa kuboresha vituo vya afya na hospitali za kuhudumia watoto wachanga na kujengwa pamoja na kusomesha wataalam wa afya," alisema Dk. Mkony.

Maadhimisho hayo yameenda sambamba na uzinduzi wa Kitengo cha Kuhifadhi na Kuratibu Maziwa ya Mama kwa kuhakikisha watoto hao wanapata maziwa ya mama zao kwa wakati kwa kuWa watoto wanaozaliwa kabla ya muda wanakuwa na uzito mdogo unaosababisha kuhitaji kiasi kidogo cha maziwa.

# Fursa kwa Tanzania mkutano G20 Brazil

**Na Romana Mallya**

MKUTANO wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Kundi la G20 kutoa fursa kwa Rais Samia Suluhu Hassan kushiriki mijadala inayolenga kuimarisha ushirikiano wa kimataifa katika mapambano dhidi ya njaa na umaskini.

Pia kuchochea maendeleo endelevu na matumizi ya nishati mbadala.

Mkutano huo utakaofanyika nchini Brazil, unaotarajia kufanyika kwa siku mbili kuanzia Novemba 18, mwaka huu,

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Sharifa Nyanga, Rais Samia amealikwa na Rais wa Brazil, Luiz Inácio Lula da Silva, na Mwenyekiti wa G20.

Taarifa hiyo ilisema Rais Samia amealikwa kushiriki mkutano wa jukwaa hilo lenye lengo la kukuza ushirikiano wa kimataifa kwenye masuala ya kiuchumi.

"Hii ni mara ya kwanza kwa Tanzania kuhudhuria katika mkutano wa G20. Mwaliko huu unatokana na heshima na ushawishi mkubwa ambao Rais Samia amejijengea katika majukwaa ya kimataifa," ilisema taarifa hiyo.

Kadhalika ilisema pamoja na mambo mengine, katika mkutano huo, Rais Samia anatarajia kushiriki mijadala hiyo na pia, kutumia jukwaa hilo linalokutanisha nchi zenye uchumi kubwa zaidi duniani kuelezea jitihada zinazofanywa na serikali kuhakikisha usalama wa chakula.

Pia kupunguza umaskini, kujenga maendeleo endelevu na kutafuta fursa za ushirikiano zitakazowaletea ustawi Watanzania kupitia sekta za uzalishaji.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, akiwa nchini humo, Rais Samia atafanya mikutano ya pembezoni na taasisi kubwa za kifedha duniani pamoja na kukutana kwa mazungumzo na wakuu wa nchi na serikali pamoja na baadhi ya nchi wanachama wa G20 akiwamo mwenyeji wake wa Brazil.

Taraifa hiyo ilisema lengo la mazungumzo hayo ni kukuza na kuimarisha uhusiano wa uwili hususan katika sekta ya viwanda, biashara, kilimo, nishati utalii pamoja na kutafuta fursa mbalimbali za ushirikiano, uwekezaji na miradi ya pamoja.

Ushiriki wa Rais Samia katika Mkutano wa G20 unalenga kuhakikisha kuwa Tanzania inaendelea kuchangia ipasavyo mijadala muhimu ya kimataifa kuhusu maendeleo duniani na kunadi sera za uchumi za kimataifa zitakazochochea maendeleo na ustawi zaidi nchini Tanzania na barani Afrika kwa ujumla.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz***




Magari yakiwa kwenye foleni kubwa katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la Kawe Bondeni, Dar es Salaam jana. Barabara hiyo, imekuwa na foleni sana kutokana na ujenzi unaoendelea wa miundombinu ya mabasi ya mwendokasi. **PICHA SABATO KASIKA**

# Serikali yasema neno kikokotoo mafao

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema uwiano wa kikokotoo kwa sekta ya umma na binafsi ni suala linalozungumzika na tayari imeelekeza Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) kuliangalia suala hilo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano mkuu wanane wa kazi wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi nchini (TUCTA) uliofanyika mjini hapa.

Ridhiwani alisema amesikia hoja ya kuhusu kutokuwapo kwa uwiano muafaka wa kikokotoo kwa sekta zote mbili.

Alisema maboresho yaliyofanyika kwa mujibu wa hoja yao, yameleta tofauti kubwa ya viwango kwa sekta ya umma kulipwa mkupuo wa asilimia 40 huku sekta binafsi ikibakia na asilimia 35.

Ridhiwani alisema serikali imeshatoa maelekezo hayo kwa taasisi hizo mbili na kwamba watakapokuwa tayari watatoa taarifa kwa shirikisho hilo kuhusu kima kilichofikiwa na msawazo ambao utakuwa umeangaliwa.

"Kwa sasa suala hili linazungumzika hivyo ni jukumu lenu kujiandaa na litakapoletwa katika ushirikishwaji muwe tayari kueleza hisia zenu," alisema.

Ridhiwani alisema katika bajeti ya 2024/25, serikali ilielekeza kufanyika mapitio viwango vya mafao kwa wastaafu na kuanzia mwezi Juni, mwaka huu, ilianza kulipa mafao ya mkupuo kwa wastaafu kutoka asilimia 33 hadi 40.

Alisema serikali imefanya ongezeko la asilimia mbili kwa pensheni kuanzia mwezi Januari, 2025.

Kuhusu kuboresha mishahara, Kikwete alisema serikali itaendelea kuiboresha na maslahi mengine kadri uchumi wa nchi utakapohimilika.

"Niwahakikishie lengo la serikali ni kuendelea kuboresha mishahara ya wafanyakazi na maslahi mengine kadri uchumi wa nchi yetu utakavyohimili vipaumbele vya Taifa.

"Ninapenda pia kuwafahamisha kuwa serikali katika kupunguza makali ya maisha imeridhia taasisi za umma kuandaa Mpango Motisha (Incentive Package) kulingana na tija na uwezo wa taasisi husika," alisema.

Waziri alisema serikali inahimiza suala la matumizi ya vyombo vya mashauriano hususani, LESCO, bodi za mishahara na mabaraza ya wafanyakazi na haitavumilia ulegevu katika kuitishwa kwa vikao hivyo kwa vile imeandaa rasilimali za kutosha kwa ajili ya vikao hivyo.

**SERA YA AJIRA KUPITIWA**

Kikwete alisema Wizara tayari imeanza mchakato wa kurejea sera ya ajira ambayo imesheeni mikakati ya kukuza ajira na mkazo mkubwa umewekwa katika mazingira wezeshi kwa ajili ya vijana kujiajiri na kuwajengea uwezo wa kuajirika.

"Hapa tunazungumzia sera ya kazi ya kujitolea, sera za ajira za muda mfupi na mrefu na sera inayotambua uwapo wa wenzetu aliosomeshwa vizuri, lakini bado wanazurura hawana kazi,"alisema.

Alikemea baadhi ya vyama ambavyo vimeendekeza migogoro ya uongozi ndani ya chama na baina ya chama na chama.

"Ninazo taarifa pia kwa baadhi ya vyama kugombea au kunyang'anyana wanachama. Hali hii haina afya katika umoja na mshikamano wenu, serikali inahitaji vyama imara vinavyoweza kushiriki kikamilifu na kwa weledi katika meza ya majadiliano," alisema.

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), Tumaini Nyamhokya alisema uongozi wake umerejesha rasilimali za shirikisho ikiwamo majengo yalikuwapo Dodoma na Arusha ambayo yatasaidia kujiimarisha kwenye mapato.

Akisoma risala ya TUCTA, Katibu Mkuu, Hery Mkunda, alisema tofauti iliyopo katika uwiano wa kikokotoo inaleta hisia za upendeleo na shirikisho linashauri milango ya mashauriano ifunguliwe ili jambo hilo lijadiliwe na muafaka upatikane.

Kuhusu ukosefu wa ajira, alisema TUCTA inapendekeza kuanzishwa kwa miradi mingi ya serikali kadri iwezekanavyo ili iajiri sehemu kubwa ya vijana wanaozunguka kutafuta wapate ajira kupitia miradi hiyo.

"Tunashauri serikali itupie macho utekelezaji wa sera ya ajira ya wageni, kwani kuna dalili za wazi za ukiukwaji wa sera hiyo.

"Ukosefu wa ajira unawaweka Watanzania katika hatari ya kutumikishwa kwa ujira mdogo na kazi zisizo za staha," alisema.

Alishauri serikali irejeshe chombo cha kusimamia na kudhibiti mifuko ya hifadhi ya jamii (SSRA) kwa kuwa wanaamini chombo hicho kina umuhimu mkubwa wa kusimamia mifuko ya hifadhi ya jamii.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Ukame ulivyobadili asili jamii ya Wamasai

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO



Mkazi wa Longido, mkoani Arusha, Jackline Filex akipanga mayai katika mashine maalum ya kuangulia vifaranga kwa ajili ya kuwauzia wananchi wenzake ambao ni wafugaji wa jamii ya Kimaasai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UTAMADUNI unaotajwa kuwa na nguvu barani Afrika sasa umetikiswa. Wakati zamani ilikuwa 'haramu' kwa jamii hiyo kufuga na kula mifugo yenye miguu miwili kama vile kuku, sasa wamegeuka kuwa walaji na wafugaji wazuri wa viumbe hao.

Vilevile, zamani jamii hiyo haikuruhusu watu wake kula mboga za majani, lakini sasa si tu ni wakulima, bali pia watumiaji wake.

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa habari hii, umebaini shida kuu ni ukame uliotokana na mabadiliko ya tabianchi, ambayo madhara yake yanatikisa si Tanzania tu bali duniani kote.

Neema Group ni moja kati ya vikundi vya ufugaji wa nyuki vilivyofanikiwa kiuchumi na kuongeza hamasa katika jamii ya Kimasai iliyoko eneo la Kimokouwa, Wilaya ya Longido, mkoani Arusha.

Losinyati Laizer, mkazi wa Kimokouwa, anasema wao ni wanufaika wa mradi wa ufugaji nyuki waliowezeshwa na Shirika la World Wildlife Fund (WWF), ili kunusuru uharibifu wa mazingira na ukataji miti ovyo.

Anasema matukio ya uchomaji mkaa, ujangili na uwindaji haramu wa wanyamapori, yamebadili maisha yao tangu walipoanza kurina asali na kuuza kila baada ya miezi mitatu.

"Katika kikundi chetu tuko watu 25 na tumepewa mizinga ya nyuki 15, ufugaji huu umetusaidia sana. Tunatarajia wiki hii kurina asali iliyoko kwenye mizinga. Makadirio yetu hapa ni kuvuna lita 1,200 za asali ambayo tukiuza tutapata Sh. milioni 1.2.

"Tutaiuza na yale mazao ya nyuki, kwa mfano masega tunayatengeneza tupate nta ili tutengeneze sabuni, dawa za kuchua, mafuta ya kupaka na dawa ya kupaka mdomo unaopasuka.

"Mradi huu wa nyuki unatunusuru sisi jamii ya kifugaji ya Kimasai tusifanye tena biashara haramu na tusifanye tena ujangili wa wanyamapori ili tuendeleze maisha yetu, tusomeshe watoto na tuajiri wengine," anasema Losinyati.

Anasema kwa sasa bei ya asali imezidi kupaa ambapo kilo moja ni Sh. 10,000 na kwa Dar es Salaam, inauzwa kati ya Sh. 15,000 hadi Sh. 20,000.

Losinyati anasema mradi huo utakwenda kupanuka kwa kuongeza wigo, kwa kuwa watajenga makazi bora na wataongeza kipato chao na kukua kiuchumi.

Mwanamke huyo anasema hajutii kuwekeza nguvu nyingi katika mradi huo, tofauti na ufugaji wa asili wa ng'ombe na mbuzi waliouzoea.

"Tunawashukuru Shirika la WWF, kupitia Mradi wa Land for Life. Hivi sasa tumeanza kunaona mabadiliko kiuchumi. Kwa kweli ukataji wa miti kwa ajili ya uchomaji mkaa umepungua, kwa sababu unajua nyuki, pia wanategemea miti kuchavusha asali.

"Lakini pia tutaendelea kutoa elimu kwa wengine wanaofanya uharibifu wa mazingira, waache na wajiingize katika biashara ya ufugaji wa nyuki na ufugaji wa kuku, ambao ni rafiki kwetu na mazingira," anasema.

Losinyati anasema nyuki wanawasaidia ndani ya mashamba yao kuchavusha mazao, kwa hiyo asilimia kubwa ya biashara haramu ya uwindaji wanyamapori na uharibifu wa mazingira umepungua, kwa sababu mradi wa nyuki umewasaidia.

Anabainisha kwamba kwa miaka mingi jamii ya wafugaji wa Kimasai ilijikita katika ufugaji mbuzi, ng'ombe na kondoo, lakini hawakuwa na ujuzi wa ufugaji nyuki wala kuku.

Mkazi Mwingine wa Kimokouwa, mama wa watoto wa tatu, Peipei Losinyati (25), anasema ufugaji wa nyuki umewasaidia wanawake kujiinua kiuchumi, sasa wanaweza kuwasomesha watoto katika shule za mchepuo wa Kingereza na shule za umma.

Pia wamepiga hatua kibiashara na wanaendeleza biashara zao ndogondogo, kutokana na fedha wanazopata kupitia ufugaji wa nyuki na kuku.

Peipei anasema biashara nyingine wanazofanya kwa kutumia kipato cha mauzo ya asali na mazao yake, ni kuuza bidhaa nyingine kama sukari, majani ya chai, mayai na chumvi huku vijijini.

Mkazi mwingine wa Kimokouwa, Nagelii Laizer (33) ambaye ni mama wa watoto watatu, anasema Shirika la WWF limekuwa msaada mkubwa wa kiuchumi ndani ya jamii yao.

"Walivyokuja kutupa mafunzo, walitaka tuwafundishe na wenzetu namna ufugaji nyuki na kuku unavyoweza kubadili maisha yetu kiuchumi.

"Tunamwona nyuki ni mdogo lakini ni mdudu ambaye ni kitega uchumi kipya cha jamii za Kimasai," anasema Nagelii.

Hadi sasa, kuna aina zaidi ya 20,000 za nyuki duniani, lakini maarufu zaidi ni; nyuki wa kazi ambao ni wa kike, waumbaji watafutaji malighafi ya asali na wa kiume, wako katika uzazi zaidi.

Tanzania ina aina mbili kuu za nyuki, nyuki wanaouma na wasiouma. Nyuki wasiouma huishi ndani ya matundu chini ya matawi makubwa ya miti, katika vichuguu vya mchwa na hata chini ya mapaa ya nyumba.

Inaaminika nyuki wasiouma, asali yao ina uwezo mkubwa kutibu maradhi kuliko ya wanaouma. Nao wako katika makundi: Nyuki wa kazi (Apis mellifera) na nyuki wa kiume (Drones).

Pia, kuna Malkia (Queen Bee), ambaye majukumu yake ni kuzalisha mayai na kuongoza 'koloni'. Anazalisha kemikali inayoitwa 'feromoni' inayowasaidia nyuki wengine kudumisha utaratibu wa 'koloni'.

Sera ya Taifa ya Ufugaji wa Nyuki ya Mwaka 1998, lengo lake ni kuimarisha mchango wa kudumu wa sekta hii, kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi na uhifadhi wa mazingira.

Inajumuisha kwa pamoja nyuki wanaouma na wasiouma, bila kujali masuala ya umiliki na usimamizi. Sera inahusu pia makundi ya nyuki wasiofugwa na wale wanaofugwa pamoja na nyuki wengine ambao hukusanya mbochi (nectar) au chavua (pollen) kama chakula chao.

Kuhusu ufugaji kuku na biashara ya kuuza vifaranga wa kuku, mjasiriamali Jackline Filex (29), mkazi wa Longido, ambaye anafanya kazi ya kuangua vifaranga kwa njia ya kisasa, anasema kazi hiyo imewafanya wasahau kuuza nyama inayotokana na shughuli za uwindaji haramu wa wanyamapori.

Anasema awali walikuwa wakiuza nyamapori zinazotoka katika ushoroba wa wanyamapori wa Kitendeni, ambao ni mapito ya wanyamapori wanaohama kati ya Hifadhi ya Taifa ya Arusha, Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro na Hifadhi ya Amboseli ya nchini Kenya, kwa ajili ya kutafuta malisho na maji.

"Ninawashukuru WWF, kwanza kwa kututoa tulipokuwa mwanzo katika uwindaji haramu wa wanyamapori, wametuelimisha tumetoka huko baada ya kutuletea mradi wa kuku na mashine za kuangulia vifaranga, ambao sasa tunanufaika nao kiuchumi kwa kuuza vifaranga vya kuku wa mayai na nyama.

"Tangu waliponiletea mashine ya kuangua vifaranga, tumeshaangua vifaranga zaidi ya 400 kwa ajili ya vikundi vya kijamii. Tukitotolewa mitetea ya kuku tunabaki nayo, tunauza mayai na tunauza majogoo," anasema.

Jackline anasema walikuwa wanapelekwa nyama za wanyamapori kwa ajili ya kuuza mitaani na kula majumbani.

"Tumegundua kwamba ni kosa kisheria, kwa hiyo sasa hivi hatufanyi tena hiyo biashara, kwa sababu kuna miradi ya kuku inalipa," anasimulia.

**WAZEE MILA WABARIKI**

Mwenyekiti wa viongozi wa mila (Leigwanani), Lekishon Mollel anasema wamebariki vijana, wanawake na wanaume kufanya biashara hiyo.

Anasema viongozi wa mila wa jamii hiyo wameridhia hilo kwa sababu ina matokeo ya haraka ya kutoa kipato cha uhakika ambacho hakipigiwi kelele kwamba kina haribu mazingira.

Anasema mradi huo utakuwa na manufaa makubwa kwa sababu huko nyuma, watu hawakujua kuhusu utunzaji wa mazingira, lakini Shirika la Kimataifa la WWF, wametoa elimu kwa jamii hiyo kuhusu utunzaji mazingira na kujikita katika ufugaji wa nyuki na kuku ambao kwao sasa ni neema.

Anabainisha kwamba kinachowafanya hivi sasa wanawake kwa wanaume kugeukia ufugaji huo, ni changamoto ya ukame na uhaba wa malisho ya mifugo yao.

Mzee mwingine wa mila na mfugaji, Saruni Olekuru Kayongo, anasema tatizo la wanyamapori wakali kama simba, chui na fisi kuvamia maboma yao ya mifugo na kuila, ni miongoni mwa sababu zilizosukuma jamii yao kujikita katika ufugaji kuku na nyuki.

**HALI ILIVYO**

Meneja Mradi wa Land for Life, unaotekelezwa na Shirika la Kimataifa la WWF, Reguli Marandu, anasema wanafanya kazi za uhifadhi katika vijiji hivyo, na wanapozungumzia uhifadhi wanaangalia mazingira na wanyamapori.

Marandu anasema kuna miradi mingi imeanzishwa kwa ajili ya kuboresha kipato cha jamii zinazoishi pembezoni mwa misitu na inatekelezwa ikiwamo kilimo cha alizeti.

Anasema pia huangalia namna gani uhifadhi unavyosaidia jamii zinazozunguka mazingira hayo ambayo wanayahifadhi.

"Dhana ya WWF, tunataka jamii zile zinazoishi katika mazingira hayo pamoja na wanyamapori na mazingira yetu vyote viwe na ustawi mzuri," anasema.

Kamishna wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Nchini (TFS), Prof. Dosantos Silayo, akizungumzia matokeo chanya ya mradi wa ufugaji wa nyuki Longido, anasema wadau hao wa ufugaji nyuki, wanapaswa kujiandaa kimkakati kutuumia mkutano wa dunia wa ufugaji nyuki (Apimondia) utakaofanyika Arusha mwaka 2027 ili kujiinua kiuchumi na kuvutia watalii.

Anasema utunzaji mzuri wa mazingira utawezesha nyuki kuzaliana kwa wingi na kuwezesha uchumi kukua.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## Mbaroni tuhuma mauaji ya bibi, wamkata titi na sehemu za siri

**Na Halima Ikunji,** TABORA

JESHI la Polisi mkoani hapa linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za kuhusika na mauaji ya Sagali Masanja (62) mkazi wa Kijiji cha Mahene, wilayani Nzega kisha kumkata titi na sehemu za siri na kuondoka navyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Richard Abwao, alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi, saa 7:00 usiku, huku chanzo kikitajwa ni imani za kishirikina.

Alisema watuhumiwa hao wanadaiwa kufanya mauaji ya bibi huyo wakimtuhumu kuwa mchawi akidaiwa kuhusika na tukio la kumroga mtoto aliyefia kisimani.

Kamanda Abwao alisema bibi huyo aliuawa kwa kukatwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili kisha wauaji kuondoka na titi moja, sehemu zake za siri na pia kuchukua begi lake la nguo.

"Baada ya kupata taarifa hizo kutoka kwa wananchi tulifika eneo la tukio na kukamata watuhumiwa watatu ambao ndio waliotuma wauaji kwenda kufanya tukio hilo," alosema Abwao.

Aliwaja watuhumiwa hao kuwa ni Lucia Mabula (36), mkazi wa Kijiji cha Mahene anayedaiwa kuwatafuta wauaji na kuwalipa Sh. 200,000 ili kutekeleza mauaji ya bibi huyo kwa madai kuwa alimroga mtoto wake mwaka 2023 na kufia kisimani.

Watuhumiwa wengine ni Makenzi Mabula (49) ambaye ni mume wa Lucia Mabula na Ramadhani Kurwa (38) wote wakazi wa Kijiji cha Mahene.

Kamanda Abwao alisema baada ya tukio hilo, wananchi waliwakimbiza watuhumiwa hao na kuwakamata wawili akiwamo mganga wa kienyeji, Sana Maganga (66) aliyekuwa akiwapaka dawa ili wasikamatwe, ambaye pia ni mama mzazi wa Shilinde Kaseko.

Alisema wengine waliokamatwa ni pamoja na Masumbuko Ngassa (33) mkazi wa Kijiji cha Segese Wilaya ya Kahama, mkoani Sinyanga na Shilinde Kaseko (30) mkazi wa Kijiji cha Seki, wilayani Nzega.

Alisema baada ya kukamatwa, wananchi wenye hasira walijichukulia sheria mkononi na kuwapa kipigo kikali kisha kuwachoma moto na kupoteza maisha.

Alisema watuhumiwa hao baada ya kukamatwa walikutwa na viungo vya binadamu ambavyo ni titi, sehemu za siri na vitu walivyokuwa wameiba.

Kamanda Abwao alitoa wito kwa wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi na kuwataka kuachana na imani za kishirikina kwa kuwa ni imani potofu na zinaongeza fitina, chuki na uhasama pia zinasababisha madhara kwa jamii.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Mwenyekiti CHADEMA Singida abwagwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Singida, Jackson Jingu, ameshindwa kutetea nafasi yake baada ya kushindwa vibaya na Diwani wa Kata ya Ntuntu wilayani Ikungi, Omari Mohamed Toto.

Kutokana na hilo, Jingu ametangaza Uchaguzi Mkuu 2025 atawania ubunge katika Jimbo la Singida Magharibi.

Katika uchaguzi huo uliofanyika juzi mjini Singida ambao pia, ulihudhuriwa na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Tundu Lissu, Jingu aliambulia kura 30 dhidi ya mpinzani wake, Toto aliyeibuka kidedea kwa kupata kura 52, huku nafasi ya tatu ikishikwa na Wilson Luta aliyepata kura tano.

Msimamizi wa uchaguzi huo Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chadema, Patrick Ole Sosopi, akitangaza matokeo hayo alisema nafasi ya Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Singida, aliyeshinda ni Samweli Maro kwa kupata kura 58 na hivyo kufanikiwa kutetea nafasi yake hiyo.

Alisema nafasi Mwenyekiti wa Baraza la Vijana wa CHADEMA (BAVICHA) Mkoa wa Singida, ilichukuliwa na Joseph Salum huku uchaguzi wa nafasi Katibu wa BAVICHA ilishindwa kufanyika kwa sababu waombaji wote kubainika hawana sifa.

Sosopi alisema nafasi ya Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA (BAWACHA) ilichukuliwa na Zaitun Jumanne na Katibu wa BAWACHA alichaguliwa Beatrice Robert.

Akizungumza baada ya kutangaza matokeo, Jingu alisema pamoja na kwamba ameshindwa kutetea nafasi yake, hawezi kuhama chama kama ambavyo wengine wamekuwa wakifanya baada ya kushindwa.

"Nitabaki kuwa mwanachama mtiifu kwa chama na nitaendelea kupambana kwa maslahi ya chama," alisema.

Mwenyekiti mteule wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Toto, alisema kazi kubwa iliyoko mbele yake ni kuhakikisha anakiunganisha chama ili kiwe kimoja na kuendeleza mapambano kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwakani.

"Uchaguzi umekwisha sasa tuvunje makundi libaki kundi moja tu la CHADEMA na nitahakikisha nalinda rasilimali za chama," alisema.

Awali, Lissu aliwataka wajumbe wa mkutano mkuu wa uchaguzi kuchagua kiongozi ambaye atakuwa mstari wa mbele katika mapambano kwa ajili ya uchaguzi ujao.




Kifaa maalum cha kuwekea chupa za plastiki zilizotumika kikiwa kimewekwa katika Kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Dar es Salaam hivi karibuni. Kwa mujibu wa abiria, kifaa hicho kimewekwa na uongozi wa Manispaa ya Ubungo, ili kuzuia utupaji taka ovyo kituoni hapo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Dk. Nchemba ataka utekelezaji ahadi ya mabadiliko tabianchi

**Na Benny Mwaipaja, Baku,** AZERBAIJAN

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Lameck Nchemba, amezitaka nchi zilizoendelea kutimiza ahadi yao ya kutoa dola za Marekani bilioni 500, sawa na dola bilioni 100 kila mwaka kwa ajili ya kuzisaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi katika kipindi cha miaka mitano, kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2025.

Dk. Nchemba alitoa kauli hiyo jana wakati akichangia hoja katika Mkutano wa Ngazi ya Juu wa Mawaziri uliojadili namna ya kupata fedha kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) unaofanyika katika Mji wa Baku, nchini Azerbaijan.

Alisema ripoti ya Mkutano wa COP28, uliofanyika Dubai mwaka jana, inaonesha kwamba kuna kasi ndogo katika kutimiza ahadi ya Mkataba wa Paris katika kuhamasisha upatikanaji ama uchangiaji wa dola 100 bilioni ambapo kuna pengo la takribani dola bilioni 60 kila mwaka hali inayo ziathiri nchi zinazoendelea katika kupanga mipango ya maendeleo.

Aidha, Dk. Nchemba alisema Tanzania inataka kuwe na uwazi katika namna fedha hizo dola bilioni 100 zinazotakiwa kutolewa kila mwaka kwa nchi zinzoendelea ili kuweka uwajibikaji kulingana na Mkataba wa Paris kuhusu suala hilo la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kuwa mabadiliko ya tabianchi ni janga linalobomoa uchumi wa nchi zinazoendelea na kushauri matamanio na ahadi zinazotolewa na mataifa makubwa yawekwe katika vitendo ili kuzinusuru nchi zinazoendelea kutokana na madhara yanayosababishwa na mabadiliko hayo ya tabianchi.

Dk. Nchemba alisema kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoendelea iliyoathirika na matokeo hasi ya mabadiliko ya tabianchi na inajitahidi kutumia rasilimali zake kukabiliana na athari hizo ikiwemo kurejesha miundombinu iliyoharibiwa na mafuriko lakini fedha hizo za ndani hazitoshelezi mahitaji.

"Pia tunatoa wito wa kupitia upya usanifu wa kifedha wa kimataifa na utaratibu wa ufadhili chini ya mkataba ili kusaidia uhamasishaji wa fedha thabiti na za muda mrefu kwa kiwango cha uwekezaji unaohitajika na nchi zinazoendelea kupambana na shida ya mabadiliko ya tabianchi" alisema.

Zaidi wa watu 50,000 wakiwemo wanadiplomasia kutoka zaidi ya nchi 200 wanachama wa Umoja wa Mataifa, wanakutana katika jiji la Baku, Azerbaijan kujadili namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutafuta vyanzo vya fedha za uhakika za kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ya kukabiliana na changamoto hizo, ikiwemo kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars nafasi ya kufuzu fainali za AFCON 2025 Morocco ipo

**TIMU** ya Soka ya Taifa maarufu Taifa Stars inatarajia kushuka dimbani leo ugenini kucheza dhidi ya Ethiopia.

Taifa Stars na Ethiopia zinakutana katika mechi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), fainali hizo zitachezwa mwakani nchini Morocco.

Timu hizo mbili ziko katika Kundi H, pamoja na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DR Congo) na Guinea.

Mechi nyingine ya kundi hilo itakayochezwa leo kuanzia saa 4:00 usiku itakuwa ni kati ya wenyeji Guinea dhidi ya DR Congo.

Tayari DR Congo yenye pointi 12 kibindoni imeshakata tiketi ya kucheza fainali hizo na katika msimamo wa kundi hilo inafuatiwa na Guinea yenye pointi sita, Taifa Stars ina pointi nne wakati Ethiopia inaburuza mkia ikiwa na pointi moja.

Kimahesabu, bila kujali au kufuatilia matokeo ya mechi nyingine, Stars inatakiwa kuvuna pointi sita katika mechi zake mbili zilizobakia.

Leo inatakiwa kuwafunga Ethiopia na baadaye kurejea nyumbani kuwasubiri Guinea na kuwachapa katika mchezo utakaofanyika Novembа 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Katika siku za hivi karibuni, Stars imekuwa na matokeo chanya inapocheza ugenini na kuwa na wakati mgumu inapopambana kwenye ardhi ya nyumbani.

Hili linawezekana kubadilika endapo wachezaji watajituma kupata ushindi wa aina yoyote leo ugenini Kinshasa na baadaye kurejea kumaliza kazi hapa nyumbani kwa kuwafunga Guinea.

Ushindi katika mechi ya leo ni muhimu sana kwa Stars kwa sababu utawafanya wachezaji wawe kwenye morali ya juu kuelekea mchezo wa mwisho wa hatua hiyo ya makundi.

Katika soka hakuna kisichowezekana, kinachotakiwa ni kuwaamini wachezaji wetu ambao wameteuliwa na Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco' kupeperusha bendera ya Tanzania kwa sasa katika mashindano hayo.

Tunawakumbusha wadau wa soka nchini wakiongozwa na viongozi na wanachama wa klabu pendwa za Simba na Yanga, kuhamishia nguvu zile wanazowekeza pale wanapokuwa na mechi zao za dabi katika timu ya taifa kwa sababu tunahitaji kupata matokeo chanya.

Dua na kutoa mawazo chanya kuelekea mechi hizi mbili ndio jambo pekee ambalo tungependa kulisikia katika kipindi hiki kwa sababu tunataka kuwa na mwendelezo wa kushiriki mara kwa mara fainali za AFCON.

Kikubwa benchi la ufundi ambalo limepewa dhamana ya kuiongoza Stars inatakiwa kufanya kazi yake kwa kujiamini na kuwaambia wachezaji wetu wanaweza, hii itasaidia kuwaongezea nguvu, kila mchezaji atakayepata nafasi ya kucheza afahamu nchi inamtegemea, aingie uwanjani kupambana kwa ajili ya Watanzania wengine milioni 60 walioko nje.

Tunawakumbusha wachezaji wa Stars kufahamu hata mbuyu ulianza kama mchicha, mastaa ambao leo hii tunawaona katika klabu mbalimbali za Ulaya, walionekana kupitia mataifa yao na kufanya vyema kwa timu hiyo kutawatafanya wao na wengine wanaochipukia.


Kila mchezaji atakayevaa jezi ya Stars ajue yuko vitani na anatakiwa kupambana bila kukata tamaa, kufanya vizuri katika mechi ya leo, kutawarahisishia kukamilisha dakika nyingine 90 zilizobakia watakapoikaribisha Guinea.

Mungu ibariki Taifa Stars, Mungu ibariki Tanzania, nafasi ya kufuzu fainali za AFCON 2025 kwa nchi yetu tunayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwango

# Gamondi ametolewa kafara Yanga, bado watatue tatizo

**KOCH**A aliyeipa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa misimu mitatu mfululizo na msimu uliopita na kuifikisha hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Miguel Gamondi, ametimuliwa.

Gamondi alichukua mikoba ya Nasreddine Nabi, alikuwa mmoja wa makocha wenye misimamo, na aliitengeneza Yanga isiyokuwa na 'abiria' uwanjani.

Kwangu binafsi ni mmoja wa makocha ambao niliokuwa nawakubali kutokana na jinsi alivyoitengeneza Yanga kutomtegemea mchezaji mmoja.

Wakati wa Nabi, Yanga iliishi kwa kumtegemea, Fiston Mayele, ambapo wachezaji karibuni wengi wa Yanga wakimzunguka yeye kwa ajili ya kupata ushindi.

Hata mashabiki wa Yanga kama siku ambayo Mayele, aliyeuzwa katika klabu ya Pyramids ya Misri, hachezi, wanakuwa roho juu na hawana uhakika wa kupata ushindi.

Alipoichukua Gamondi alitengeneza mfumo ambao kila mchezaji alikuwa anamsaidia mwenzake.

Yanga ilikuwa ikikabia juu. Mastraika licha ya kufunga mabao walikuwa na kazi ya kuwafanya mabeki wa upinzani wasiwe huru na mipira.

Yanga ilikuwa inacheza mpira kwa kasi na hakukuwa na mfungaji mmoja. Si lazima straika akufunge.

Yeyote aliweza kufunga na kwa wakati wowote. Yanga iliogopeka siyo hapa nchini tu hata nje ya Tanzania.

Hiyo ndiyo Yanga na Gamondi, ambaye jana klabu hiyo ilitangaza rasmi kuachana naye.

Yote haya ni kutokana na vipigo viwili mfululizo vya bao 1-0 dhidi ya Azam FC na 3-1 dhidi ya Tabora United.

Hata hivyo yapo mengi yanazungumzwa na watu kutoka ndani ya Yanga kulikuwa na kutoelewana na viongozi kwa madai kuwa ni mbishi.

Mfano wengine wanasema hamtumii beki, Kibwana Shomari, kwa sababu zisizoeleweka na alifanya hivyo licha ya Yao Kouassi kuwa mgonjwa, aliamua kumtumia, Denis Nkane, ambaye si eneo lake.

Wanaomtetea kocha huyo nao wamedai Gamondi alianza kuingia kinyongo katika usajili wa dirisha kubwa, baada ya kuletewa wachezaji ambao hawakuwa chaguo lake.

Wachezaji hao ni Clatous Chama na Jean Baleke, huku mwenyewe akielekeza wasajiliwe wachezaji ambao hawakusajiliwa.

Binafsi hadi sasa sijaona sababu hasa ya viongozi wa Yanga kumtimua kocha huyo. Na ndiyo sababu hata uongozi haujasema sababu hasa ya kuchukua uamuzi huo. Sidhani kama tatizo la kutofanya vyema katika michezo miwili ya Ligi Kuu ndio msingi wa Gamondi kutemwa.

Ukiangalia tangu kuanza kwa msimu huu, Yanga imepoteza ule uchezaji wake uliozoeleka na ilionekana iko karibu kupoteza mechi kuliko kushinda, kila ilipokuwa ikicheza mchezo mmoja.

Na kupoteza mechi mbili kumechangiwa mno na makosa ya kibinadamu ya waamuzi, la sivyo ingekuwa imepoteza mechi nyingi zaidi ya hizo mbili.

Ninavyoona mimi tatizo lipo kwa wachezaji wa Yanga ambao walikuwa kwenye kiwango cha juu msimu uliopita, lakini msimu huu kimepungua.

Wachezaji kama Stephane Aziz Ki, Pacome Zouzoua, Clement Mzize, Kennedy Musonda na wengine waliokuwa mhimili wa Yanga, msimu huu hawajaanza wakiwa na makali yao.

Imedaiwa pia baadhi ya wachezaji wa timu hiyo wamevimba 'vichwa' kutokana na umaarufu, hivyo kujiingiza katika starehe, hali inayosababisha viwango vya vipungue.

Mimi nadhani viongozi wa Yanga, wangemsaidia kocha kwa kusajili wachezaji ambao wangekuja kuisukuma hapo ilipo kwenda mbele.

Viongozi wa Yanga wangeanza kuangalia kuwaondoa baadhi ya wachezaji ambao wamekuwa na majina makubwa lakini mchango wao kwa sasa ni mdogo na kusajili wengine kama walivyofanya watani zao wa jadi Simba, badala ya kumtimua Gamondi.

Nina uhakika kama Gamondi angepata wachezaji wenye umri mdogo kama wale waliopo Simba, angeitengeneza Yanga ambayo ingekuwa na kasi zaidi kuliko hata hii tuliyoiona msimu uliopita.

# GCLA yapiga marufuku biashara kemikali kwa wasiosajiliwa

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imewaonya wauzaji wakubwa wa kemikali kuacha kuwauzia wauzaji wa kati na wadogo wa kemikali ambao hawajasajiliwa kufanya biashara hiyo.

Mkurugenzi wa Huduma za Udhibiti wa GCLA, Daniel Ndiyo aliyasema hayo wakati wa kikao na wadau wanaojihusisha na uingizaji na usambazaji wa kemikali bashirifu, kilichofanyika Ofisi za Kanda ya Mashariki jijini Dar es Salaam.

"Wadau wote wa kemikali lazima wawe wamesajiliwa na mamlaka hii kwa mujibu wa sheria pamoja na kutimiza maazimio tuliyoweka ili waweze kufanya biashara zao kwa usalama, kulinda afya za binadamu na mazingira," alisema Ndiyo. Kamishna Msaidizi wa Sayansi Jinai kutoka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Ziliwa Machibya alisema kemikali bashirifu ni hatari katika mazingira ya matumizi ya dawa za kulevya.

Aliwawasihi wadau wa kemikali bashirifu kufuata taratibu za usajili ili ziweze kutumika katika matumizi yaliyokusudiwa katika uzalishaji mbalimbali na kwa usalama. Geoffrey Jato, ambaye ni mdau wa kemikali aliipongeza mamlaka kwa kuwapa elimu na kuendelea kuweka ushirikiano wa karibu na wadau wa kemikali jambo ambalo limeweza kuwatatulia changamoto mbalimbali zikiwamo za usajili.

"Elimu tuliyoipata ya usajili wadau wengi hawakuwa nayo ila kwa sasa, wingi utaongezeka wa wadau kujisajili na kupata elimu ili wanapofanya manunuzi ya kemikali au uzalishaji waweze kufanya kwa usalama," alisema Jato.



Wajasiriamali wadogo na wakati wakipata mafunzo kutoka kwa Ofisa mikopo wa benki ya TIB, Eugen Ingwe (kushoto), wakati wa semina ya siku moja, iliyoandaliwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda vidogo (SIDO), jijini Dar es Salaam juzi, kwaajili ya kuwajengea uwezo na kuwaelekeza fursa za mikopo inayotolewa na benki hiyo kupitia dirisha dogo la uwekezaji nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bilioni 12/- kusaidia utafiti MUHAS

**Na Grace Mwakalinga**

CHUO Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kimepokea ruzuku ya Sh. bilioni 12.5 kutoka Sweden kupitia Shirika la Maendeleo (SIDA).

Fedha hizo ni kwa ajili ya kufundisha wataalam wa afya katika ngazi ya Shahada ya Uzamili na Uzamivu, kufanya utafiti na kuboresha ubunifu.

Akizungumza juzi wakati wa hafla ya utiaji saini wa mkataba huo katika Kituo cha Umahiri wa Moyo na Mishipa ya Damu kilichoko Mloganzila, jijini Dar es Salaam, Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Appolinary Kamuhabwa, alisema mkataba huo utadumu kwa miaka sita, kuanzia Desemba 2024 hadi Juni 2030.

Alisema hatua hiyo ni ushirikiano ulioko kati yao na Sweden, ulioanza tangu mwaka 1980, ukilenga kukuza utafiti na mafunzo ya wataalam wa afya na kutoa fursa kwa wanafunzi kuchangia ubunifu na uvumbuzi.

Prof. Kamuhabwa alisema MUHAS itashirikiana na vyuo vikuu vitatu vya Sweden ambavyo ni Umeå, Karolinska, na Uppsala ambapo wanafunzi watakaonufaika na programu hiyo, watapata fursa ya kutuma sampuli za utafiti na kusoma baadhi ya masomo kwenye vyuo hivyo.

Alisema matokeo ya ushirikiano wao tayari yameleta mafanikio katika kuboresha miongozo, mifumo, na sera zinazohusiana na sekta ya afya.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, anayeshughulikia Utafiti na Uvumbuzi, Prof. Bruno Suguya, alisema mradi huo utatekelezwa kwa hatua tofauti.

Alisema kila mwaka programu mbalimbali zitafanyika chini ya usimamizi wa pamoja kati ya MUHAS na vyuo vya Sweden.

Alisema ripoti za utekelezaji wa mradi zitawasilishwa katika Ubalozi wa Sweden na kupitiwa na Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA) kwa ajili ya kupitishwa.

Alisema ruzuku hiyo itajikita kutekeleza utafiti katika magonjwa ya Malaria, Kifua Kikuu, huduma za mama na mtoto na maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI

"Tunaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya utafiti katika sekta ya afya kwa ushirikiano na Sweden, na tunapata hati safi katika maeneo kama ukaguzi wa mahesabu na utoaji wa mafunzo bora," alisema Prof. Suguya.

Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Dk. Harrison Mwakyembe, alisema MUHAS imekuwa moja ya taasisi kinara inayotoa ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za sekta ya afya nchini kupitia utafiti wake.

"Kwa miaka minne nikiwa Mwenyekiti wa Bodi, nimeona utafiti mahiri unaofanywa na chuo hiki, tuna uhakika kwamba fedha hizi zitaleta bunifu nyingi zaidi katika kutatua matatizo ya afya nchini," alisema Dk. Mwakyembe.

Alisema MUHAS kwa mara nyingine, inanufaika na ufadhili kutoka Sweden kwa ajili ya kuimarisha utafiti katika maeneo nyeti ya sekta ya afya.

Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Charlotta Macias, alisema ushirikiano wa Tanzania na Sweden katika utafiti wa sekta ya afya umeanza miaka 48 iliyopita na umelenga kuongeza uwezo wa MUHAS kushughulikia changamoto zilizoko katika sekta ya afya, rasilimali watu, sera na magonjwa.

Alisema wanatarajia MUHAS itaendelea kutoa mafunzo ya utafiti wa kiwango cha juu kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya nchini na kwamba ufadhili huo utaimarisha zaidi juhudi za chuo hicho katika kuzalisha wataalamu wabobezi.

Wakati wa ufunguzi wa kongamano la kidigitali katika sekta ya afya lililofanyika eneo la Mloganzila, Waziri wa Afya, Jenista Mhagama alisema, katika kipindi cha miaka mitatu, serikali imetumia Sh. trilioni 6.2 kuboresha sekta hiyo.

Alisema uboreshaji huo umehusisha ujenzi wa miundombinu ya utoaji huduma, ununuzi wa vifaa tiba, ikiwamo vya uchunguzi na dawa ili huduma za afya kuwafikia wananchi wengi.

Akielezea umuhimu wa kukuza utaalamu na utafiti, Waziri Mhagama alisema MUHAS inatoa wataalam wabobezi ambao wamesaidia kuimarisha huduma za afya nchini.

Alisema amefurahishwa na teknolojia inatumiwa na Sweden katika kutoa taarifa za viashiria ya ugonjwa wa saratani ya matiti na kizazi kwa kina mama.

Alisema teknolojia hiyo ina uwezo wa kutoa taarifa za mgonjwa kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali.

Waziri Mhagama alisema wamejipanga kutumia ubunifu huo ili kusaidia utoaji wa huduma za awali kwa wagonjwa wanaobainika mapema kuwa na viashiria vya saratani.

# Wahimiza matumizi nishati safi kupikia

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, ametoa wito kwa serikali, sekta binafsi na washirika wa maendeleo kuunga mkono ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa manufaa ya watu waishio barani Afrika.

Dk. Nchemba alitoa wito huo wakati akifunga mkutano uliojadili umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia, kwa niaba ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango.

Alisema hayo pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29), unaofanyika katika Mji wa Baku, nchini Azerbaijan.

Alisema ni muhimu kwa nchi za Afrika kutekeleza sera zinazochochea kasi ya matumizi ya teknolojia za nishati safi ya kupikia na kutenga fedha za kutosha kuisaidia jamii husussan iliyoathirika zaidi na athari hasi ya mabadiliko ya tabianchi.

"Ni muhimu kujenga ushirikiano unaolenga kuongeza ujuzi na utaalam ili kuwa na suluhisho la changamoto ya matumizi duni ya teknolojia ya kuwezesha matumizi ya nishati safi ya kupikia kupatiwa ufumbuzi wa kudumu" alisema.

Alilisisitiza umuhimu wa wadau wote kushirikiana ili kuweka mazingira wezeshi ya mipango ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kujenga mustakabari na kesho iliyobora kote barani humo.

Mkutano huo wa nishati safi ya kupikia uliandaliwa na Tanzania kwa kushirikiana na Umoja wa Afrika (AU) pamoja na Tume ya Nishati Afrika (AFREC) uliyofanyika pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29).

Zaidi wa watu 50,000 wakiwamo wanadiplomasia kutoka zaidi ya nchi 200 wanachama wa Umoja wa Mataifa, wanakutana katika Jiji la Baku, nchini Azerbaijan.

Wamekutana kujadili namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kwa kutafuta vyanzo vya fedha za uhakika za kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ya kukabiliana na changamoto hizo, ikiwamo kuhimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

HABARI KITAIFA

# Wadau duniani kujadili mustakabali sekta madini

**Na Mary Geofrey**

WIZARA ya Madini imeandaa mkutano wa kimataifa wa uwekezaji utakaojumuisha washiriki 1,500 kutoka mataifa mbalimbali duniani, utakaofanyika kwa siku tatu kuanzia Novemba 19, mwaka huu.

Lengo la mkutano huo ni kujadili kwa pamoja mustakabali wa sekta ya madini, kushirikishana maarifa, ujuzi kuangazia fursa mpya zinazojitokeza katika sekta hiyo na kuimarisha mazingira ya uwekezaji kwa mataifa mengine duniani.

Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo ambao pia, utatoa nafasi kwa washiriki kujifunza kuhusu sera na mikakati mipya ya serikali.

Alisema mkutano huo unaotarajiwa kufunguliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, utajadili masuala ya kisheria na kushuhudia teknolojia mpya na ubunifu unaoweza kuleta thamani zaidi katika utafiti.

Alisema pia, katika uchimbaji na uongezaji thamani wa madini kupitia mawasilisho na maonyesho katika mabanda yanayoenda sambamba na mkutano.

"Mkutano huu unalenga si tu kuvutia uwekezaji, bali pia kuweka msingi thabiti wa ushirikiano baina ya wadau, kuimarisha uzalishaji wa madini, na kuhakikisha kuwa rasilimali hizi zinawanufaisha watanzania kiuchumi na kijamii," alisema Mavunde.

Kadhalika alisema kupandisha thamani ya madini yanayozalishwa nchini kabla ya kusafirishwa nje kwa lengo la kuchochea uanzishwaji viwanda vitakavyokuwa na manufaa nchini, kwa nchi jirani na duniani.

"Mkutano huu utaambatana na hafla ya usiku ya madini, tukio maalum la kutambua mchango wa wadau waliofanya vizuri katika sekta ya madini kupitia makundi mbalimbali.

"Kutambua mchango wa wadau hawa katika maendeleo na ukuaji wa sekta, huku ikihamasisha wadau wengine kuongeza juhudi, kuziona fursa zilizopo na kuchangia katika mafanikio ya sekta ya madini nchini. Pia, usiku wa madini huambatana na onesho la bidhaa za madini ya vito," alisema Mavunde.

Alisema kwa mara ya kwanza mwaka huu, wataonesha aina nyingine za madini yakiwamo ya viwandani na ujenzi kwa lengo kuangazia fursa zilizoko na kutambua matumizi ya madini katika maisha ya kila siku ya kiuchumi na kijamii.

"Pia liitaangalia namna madini yanavyojifungamanisha na sekta nyingine kutoka viwandani hadi katika matumizi ya kawaida na namna yanavyochochea maendeleo kwa Watanzania na ulimwengu kwa ujumla," alisisitiza.

Mkutano huo unaoongozwa na kaulimbiu isemayo, 'Uongezaji thamani Madini kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii' inayolenga kuhimiza umuhimu wa uongezaji thamani wa madini kama njia ya kuleta faida zaidi za kiuchumi na kijamii kwa maendeleo endelevu ya taifa na dunia.



Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (wa pili kulia), akikabidhi tuzo kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya NIDA, Hamza Haji Rafiq, wakati wa utoaji wa Tuzo za Rais za Mwaka kwa Wazalishaji Bora, zilizoandaliwa na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI), Dar es Salaam hivi karibuni. Kulia ni Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mabehewa 264 ya mizigo SGR kuja mwezi ujao

**Na Jenifer Gilla**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRA) linatarajia kupokea mabehewa 264 ya mizigo yatakayotumika katika Reli ya Kiwango cha Kimataifa (SGR) kwa ajili ya shughuli za usafirishaji nchini.

Mabehewa hayo ni sehemu ya 1,430 ambayo serikali iliyaagiza kutoka katika kampuni ya China inayojulikana kama CRRC kwa ajili ya kuendeleza huduma ya reli ya kisasa.

Taarifa iliyotolewa na TRA jana ilieleza kuwa meli iliyobeba mabehewa hayo imeng'oa nanga nchini China Novemba 12, mwaka huu na inatarajiwa kufika nchini mwezi ujao.

"Katika mzigo huo, kuna mabehewa 200 ya kubeba makasha ya makontena, na mabehewa 64 ya kubeba mizigo isiyofungwa" ilisema taarifa hiyo.

Mwaka 2022, TRL ilisaini mkataba wa miezi 12 na Kampuni ya CRRC uliogharimu Dola za Marekani milioni 127.2 kwa ajili ya kutengeneza mabehewa hayo na kuyaleta nchini.

Lengo la mabehewa hayo ni kusafirisha mizigo ili kupunguza msongamano barabarani na kurahisisha usafirishaji wa ndani na nje ya nchi.

# DIT yageukia mafunzo akili mnemba

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), imedhamiria kutoa mafunzo ya kisasa ya akili mnemba (AI) kwa vijana wengi wa Tanzania kwa kujenga kituo cha umahiri cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano chenye maabara 20.

Mhadhiri wa taasisi hiyo, Dk Joseph Matiko, alisema hayo juzi wakati ujumbe wa Benki ya Dunia (WB), ulipotembelea mradi wa RAFIC unaotekelezwa katika taasisi hiyo.

Matiko ambaye pia ni msimamizi wa ujenzi wa mradi wa kituo hicho chenye majengo mawili, alisema maabara hizo 20 zitakuwa na vifaa vya kisasa vya kufundishia masuala ya teknolojia.

Alisema akili bandia imekuwa habari ya dunia hivyo wameona ni muhimu kuweka mkazo kwenye mafunzo hayo ili Tanzania isiachwe nyuma na ulimwengu unaokwenda kwa kasi kwenye eneo la teknolojia.

"Wote ni mashuhuda kwa namna ambavyo matumizi ya akili bandia (AI) yanavyoenea kwa kasi duniani kwa hiyo na sisi tumeona twende na kasi hiyo kwa kuhakikisha vijana wengi wa Tanzania wanakuwa na elimu hiyo," alisema.

Alisema mbali na akili bandia pia kituo hicho cha umahiri kitakuwa mahsusi kwa ajili ya kufundisha masuala ya usalama wa mitandao na teknolojia mbalimbali lengo ikiwa ni kuwajengea uwezo na ujuzi vijana ili waweze kujiajiri au kuajiriwa.

Alisema lengo la serikali ni kuweka mazingira vijana kuwa na ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira ili waweze kuwa na mchango mkubwa kwenye maendeleo ya uchumi wa nchi yao.

"Mpaka sasa ujenzi umefikia asilimia 85 na vifaa vimeshaanza kununuliwa na wanafunzi wameshaanza kunufaika na ujenzi ambao utagharimu Sh. bilioni 22," alisema.

Katika hatua nyingine, alisema DIT imekuwa ikiwafuatilia wanafunzi wake wanaohitimu wanapokwenda sokoni wanafanya shughuli gani baada ya kuhitimu.

Alisema kila mwaka wamekuwa wakifanya hivyo kujua wahitimu wao wanafanya nini na kama elimu waliyoipata wanaitumia kwa kijiajiri au kuajiriwa na kampuni mbalimbali.

"Kila mwaka tunafanya inaitwa (Tracer Study) na ya mwaka jana imetuonyesha kuwa zaidi ya asilimia 75 ya wahitimu wetu aidha wamejiajiri au kuajiriwa na kampuni mbalimbali kwa hiyo tunaona fahari kuwa tunachofundisha kinaleta tija kwa taifa," alisema.

Kuhusu kutengeneza Satellite, alisema DIT imekuwa mstari wa mbele kuendeleza teknolojia mbalimbali hivyo wamekuwa wakifanya jitihada za kuhakikisha satellite inakamilika na inarushwa hewani.

"Sasa hivi tuko kwenye hatua ya matengenezo ya satellite baadaye tutaenda kwenye majaribio kwa kusaidiana na wataalamu mbalimbali watatusaidia kuipeleka huko angani inakotakiwa kuwa ili tuwe na satellite yetu ya kwanza Tanzania," alisema



## BMH kuvuna figo bila ya upasuaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamini Mkapa (BMH) imeanza kufanya uvunaji wa figo kwa njia ya matundu bila kumfanyia mtu upasuaji mkubwa.

Upasuaji huo kwa njia ya matundu (Laparoscopic Nephrectomy) unafanywa kwa ushirikiano na wataalam kutoka Shirika la ZGT Overzee la Uholanzi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa mfumo wa mkojo na Upandikizaji Figo, Reuben Mkinga, alisema huduma hiyo inatolewa bila kufanya upasuaji kwa mtu anayetoa figo kwa mgonjwa mwenye matatizo ya figo.

Alisema upasuaji huo ni tofauti na ule waliokuwa wakifanya mwanzo kwa kuwa wanatumia matundu madogo kutoa figo ,isipokuwa chini ya kitovu kunakuwa na tundu refu kidogo kwa ajili ya kuitoa figo yenyewe.

"Huduma hii ya kuvuna figo bila upasuaji kutoka kwa mtu anayetoa figo ni mara ya kwanza kufanyika hapa BMH, toka ilipoanzisha kitengo cha huduma ya upandikizaji figo," alisema Dk. Mkinga.

Alisema faida ya upasuaji huo ukilinganisha na ule wa zamani ni kwamba, mtu anayetoa figo anakuwa hana maumivu makubwa baada ya upasuaji.

Daktari huyo alisema anapotolewa, uponyaji wake unakuwa wa haraka zaidi ukilinganisha na yule aliyetolewa figo kwa kupasuliwa upande wa ubavu.

Alifafanua zaidi kuwa aliyepasuliwa chini ya mbavu anakuwa na mshono mkubwa na kidonda huwa kikubwa, hata uponaji wake unakuwa wa muda mrefu kidogo, ukilinganisha na mgonjwa aliyetumia upasuaji kwa njia ya matundu madogo.

Alisema mgonjwa aliyepasuliwa kwa njia ya matundu madogo, hukaa hospitalini kwa muda mfupi kati ya mbili hadi tatu, lakini yule aliyefanyiwa kwa njia ya upasuaji wa chini ya mbavu hutumia muda mrefu kukaa kuanzia wiki moja hadi mbili kabla ya kuruhusiwa.

Alieleza BMH imeanzisha huduma ya uvunaji figo bila ya upasuaji, ili kuishawishi jamii kuwatolewa figo watu wenye uhitaji pale wanapokuwa na tatizo la figo.

Mkazi wa Mbeya, Jane Mwandete, ambaye alijitolea kumchangia figo kaka yake, alisema tangu amefanyiwa upasuaji wa aina hiyo anaendelea vizuri na kuishukuru serikali kwa kuanzisha huduma hiyo.

Mkuu wa Idara ya Kitengo cha Moyo wa BMH na Daktari Bingwa mbobezi wa magonjwa hayo, Dk. John Meda, alisema tangu kitengo cha magonjwa ya moyo kuanzishwa hospitalini hapo wamepandikiza vianzisha mwendo kwa wagonjwa zaidi ya 30.

Alisema huduma hiyo wanaifanya kwa ushirikiano na madaktari kutoka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) na kuhimiza jamii kujitokeza kwa wingi kufanya vipimo vya awali ili kujua kama wana tatizo la moyo.

# Vifo magonjwa yasiyoambukiza vyaongezeka

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema vifo vitokanavyo na magonjwa yasiyoambukiza nchini vimeongezeka kufikia asilimia 33 mwaka 2023, kutoka asilimia 20 kwa mwaka 2020.

Mkurugenzi wa Rasirimali Watu na Utawala wa Wizara ya Afya, Issa Ng'imba, alibainisha hayo jana, jijini Dodoma, wakati akifunga kikao kazi cha watunga sera na watawala kutoka wizara 15 za kisekta.

Alisema magonjwa yasiyoambukiza kama shinikizo la damu, saratani, magonjwa ya kinywa na meno, kisukari na changamoto za afya ya akili yanazidi kuongezeka, hivyo yanahitaji hatua za haraka na za pamoja.

"Magonjwa haya ambayo yanachangia kiwango kikubwa cha vifo na kupunguza ubora wa maisha ya watu yameathiri familia, jamii na uchumi kwa ujumla. "Hivyo basi ni jukumu letu kuhakikisha tunaweka sera na mikakati thabiti ili kuzuia, kugundua mapema na kutibu magonjwa haya," alisema.

Aidha, alisema kutokana na ukubwa wa tatizo hilo nchini kuna haja ya kuongeza elimu umma kuhusu njia za kuzuia magonjwa yasiyoambukiza kwa kuhimiza mabadiliko ya mtindo wa maisha kama kufanya mazoezi mara kwa mara.

Pia, kuimarisha mifumo za huduma ya afya ili iweze kutoa huduma bora na zinazoweza kupatikana kwa urahisi hususani kwa wanaoishi vijijini na wasiokuwa na uwezo wa kifedha.

"Kuwekeza katika utafiti na takwimu ili kutathmini kwa usahihi hali ya magonjwa yasiyoambukiza na kupima ufanisi wa mikakati tunayoweka, kuhusisha sekta binafsi na mashirika ya kiraia katika kufanikisha juhudi za kudhibiti magonjwa haya," alisema.

Akizungumzia kikao hicho, Ng'imba alisema kinalenga kuimarisha mikakati ya kudhibiti ongezeko la magonjwa yasiyoambukiza ambayo yameendelea kuwa tatizo kubwa duniani.

"Majadiliano yanaonesha tunaweza kupunguza mzigo wa magonjwa haya kupitia utashi wa kisiasa, ufadhili wa kutosha na kuhamasisha wadau wote kushiriki, kwa pamoja tunaweza kuleta mabadiliko chanya kwa jamii yetu, "alisema

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Wizara ya Afya, Dk. Hamad Nyembea, alisema kikao hicho cha siku mbili kilikuwa na lengo la kuiimarisha mikakati ya kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza.

"Katika kikao hichi cha siku mbili tumejadili namna ya kuimarisha mikakati mbalimbali ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza, lakini tumeshirikisha pia wizara ambapo takribani wizara 15 zimeshiriki."

"Lengo la kushirikisha wizara ni kutokana na tatizo hilo ni mtambuka ambalo linahitaji ushiriki wa wizara zote kukabiliana nalo hivyo kila wizara ikitekeleza majukumu yake kikamilifu tutafanikiwa kudhiti tatizo hilo, "alisema

Hata hivyo, alisema katika kikao hicho wametoka na maazimio saba ambayo wanakwenda kutekeleza ikiwamo kuwa na vikao vya mara kwa mara



Dk. Doreen Gasper (kushoto) kutoka Taasisi ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI), mkoani Dar es Salaam, akimhudumia Fausta Mbuya wakati wa kambi ya matibabu ya magonjwa yasiyoambukiza, iliyoandaliwa na Wizara ya Afya, katika viwanja vya Nyerere Square, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wadhibiti ubora wakumbushwa kuzingatia wajibu wao sekta elimu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imewataka Wathibiti Ubora wa Shule nchini kutekeleza wajibu wao ipasavyo ili serikali iweze kufikia malengo ya kuboresha sekta ya elimu nchini.

Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora wa Shule kutoka wizara hiyo, Ephraim Simbeye, alisema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya utekelezaji wa kiunzi cha ujumuishi wa shule za awali na msingi yanayofanyika mjini Singida na kuwashirikisha washiriki 378 kutoka halmashauri 92 nchini.

Simbeye ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, alisema wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) zimepewa dhamana ya kuweka shabaha na mikakati itakayoiwezesha sekta ya elimu inafikia malengo yake.

Alisema Tanzania imejitolea kutekeleza utoaji wa elimu bora na jumuishi katika ngazi zote za elimu kutokana na kutambua umuhimu wa elimu wa wote.

"Dhamira hii inadhihirisha na kuridhia kwa vyombo mbalimbali vya kimataifa kuhusu elimu jumuishi hasa SGDs 2030 na agenda ya 2063," alisema.

Aliwataka watakapotejea katika vituo vyao vya kazi wakasimamie progamu hiyo na kuhakikisha kila mthibiti ubora wa shule aliyepata mafunzo, anakwenda katika shule za awali na msingi.

"Mhakikishe orodha inaletwa kwenu kwa kila halmashauri ili kufanya tathmini na kutoa mrejesho kwa usahihi kwa ajili ya kufanya marekebisho kwa shule," alisema.

Nao, washiriki wa mafunzo hayo walisema, yatawawezesha kutekeleza vyema majukumu yao na hatimaye shule zote kuwa jumuishi na kuondoa tatizo la mdondoko.





# Polisi wakumbushwa kuheshimu haki za raia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISHNA wa Jeshi la Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad, amewakumbusha askari wa jeshi hilo waliohitimu mafunzo ya uongozi ngazi ya cheo cha sajenti, kutekeleza majukumu yao kwa kuheshimu na kulinda haki za kila mtu kama ilivyoelezwa katika katiba ya nchi.

Aliwataka kusimamia haki na kujiepusha na uporaji wa haki kinyume cha sheria, kujiepusha na ukamataji holela wa raia, matumizi ya nguvu kupita kiasi kwa sababu matendo hayo ni kinyume na maadili ya jeshi la polisi.

Akizungumza jana wakati akifunga mafunzo hayo katika Chuo cha Polisi Zanzibar, Kamishna huyo alisema nidhamu ya kazi ndio msingi wa mafanikio hivyo ni vyema kuiweka mbele na kujiepusha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili.

Aliwasisitiza kujiepusha na vitendo vya rushwa upendeleo, matumizi mabaya ya mamlaka, kuacha kutekeleza majukumu ya msingi, mfano kwenda kusuluhisha kesi za jinai katika vituo vya polisi, kugeuza kesi za jinai kuwa za madai na kulazimisha kesi za madai kuwa za jinai.

Alisema wanapokea malalamiko kwamba raia anapofika katika vituo vya polisi kulalamika hawapewi majibu mazuri ambapo ni kinyume na maadili ya Jeshi la Polisi.

Pia baadhi ya askari huchagua kesi za kushughulikia kwa sababu ya maslahi binafsi na kuzipuuza kesi nyingine kwa visingizio kadhaa.

Alitolea mfano makosa mengi hivi sasa, utendaji wake yanahusisha vifaa vya kieletroniki kama simu za mkononi, lakini baadhi ya wapelelezi wakidai fedha kwa kisingizio cha kutafuta ushahidi wa kieletroniki kutoka kwa walalamikaji au kuacha kabisa kuzishughulikia kesi hizo.

"Niwaonye askari wachache wenye tabia hizo waache mara moja kwa sababu watakaobainika tutawashughulikia ipasavyo bila ya huruma kwa mujibu wa sheria.

"Niwaombe wananchi watupe ushirikiano, niwaahidi kwamba malalamiko yote yenye ushahidi dhidi ya askari mwenye vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili ya Jeshi la Polisi au kinyume na cha sheria, watupe ushirikiano na tutawashughulikia kwa mujibu wa sheria," alisema.

Kamishna huyo aliwataka askari kuzingatia kuwa usalama na amani inawezekana pale haki za kila mtu zinapoheshimiwa na kufanya hivyo wataongeza imani ya wananchi kwa jeshi hilo na kujenga uhusiano mzuri kwa jamii.

"Niwakumbushe hata katika mafundisho ya dini, kulinda na kusimamia haki, heshima na usawa kwa watu wote ni mambo yanayosisitizwa," alisema Kamishna huyo.

Alisema wananchi wanaofika katika vituo vya polisi kuleta malalamiko yao, wanaolalamika kuonewa ni vyema kuwasikiliza na kufanya uchunguzi ili kusaidia vyombo vyengine kutenda haki.

Pia aliwataka askari wote kutambua mfano bora wa uwadilifu, kujituma na kuheshimu sheria na kanuni za Jeshi la Polisi, ndio utamaduni wao.

Mkuu wa Chuo cha Polisi Zanzibar, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Moses Fundi, alisema mafunzo hayo yametolewa muda mwafaka wa kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu na Uchaguzi Mkuu, 2025.

Alisema jumla ya askari 1,015 kutoka mikoa yote ya Tanzania wamepata mafunzo hayo ya miezi miwili ambapo kati ya hao, askari wa kike ni 269.

Alisema kati ya wanafunzi hao, waliofaulu ni 946 na 69 wameshindwa kukidhi vigezo na kuwataka kuendelea kujiheshimu na kutunza nidhamu zao vyenginevyo wanaweza kupoteza sifa za kupandishwa vyeo.



Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad (kushoto), akikabidhi kifimbo cha heshima kwa Askari polisi wa kike, Koplo Violet Temba, baada ya kuwa mmoja kati ya askari tisa waliofanya vizuri zaidi katika mafunzo ya uongozi ngazi ya cheo cha sajini, wakati wa ufungaji wa mafunzo, katika Chuo cha Polisi Zanzibar, juzi. Jumla ya askari 1,015 walihitimu mafunzo hayo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## SMZ yafanya mageuzi makubwa sekta afya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Zanzibar imefanya mageuzi makubwa katika sekta ya afya kwa kuboresha huduma za afya ikiwamo vifaa tiba na kuendelea kuwasomesha wafanyakazi ili kuwa na mabingwa na wabobezi watakaotoa huduma bora za afya kwa wananchi wote wa mijini na vijijini.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla aliyasema hayo katika ufunguzi wa mkutano wa majadiliano wa wadau wa maendeleo, kuhusu ugharamiaji wa huduma za afya Zanzibar, kwa lengo la kufikia adhma ya afya bora kwa wote uliofanyika visiwani humo. Alisema katika kuhakikisha serikali inatoa huduma bora za afya kwa wananchi wote, imeamua kufanya uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya afya ikiwamo kujenga hospitali 10 kila wilaya pamoja na kuweka wataalamu bingwa ili kuimarisha huduma bora za afya kwa wananchi.

Alisema ili kufikia adhma ya afya kwa wote, serikali imeimarisha hali ya upatikanaji wa dawa nchini, upatikanaji wa chakula kwa wagonjwa sambamba na kuongeza wigo wa utoaji wa matibabu kwa wananchi kama vile huduma ya usafishaji wa figo.

Alisema wananchi walilazimika kutumia gharama kubwa za matibabu hayo na wengine kupoteza maisha kutokana na kukosa fedha za kugharamia huduma.

Hemed alisema serikali imeimarisha vifaa vya uchunguzi ikiwamo Xray, CT-Scan, Ultra Sound na vifaa mbalimbali vya maabara pamoja na kuboresha vifaa tiba kwa kujengwa mitambo miwili ya hewa tiba katika Hospitali ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Lumumba ambayo itatumika katika hospital za Zanzibar. Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya afya kwa kuajiri wafanyakazi wapya 1,566 kwa mwaka huu wa fedha, kujenga hospitali za mkoa, Hospitali ya Rufani ya Binguni pamoja na kutoa fursa kwa wafanyakazi wa afya kujiendeleza kielimu.

Alisema serikali inaendelea kufanya mageuzi katika mfumo wa kugharamia huduma za afya ikiwamo kuanzisha mfumo wa huduma za afya Zanzibar chini ya Sheria Namba Moja ya Mwaka 2023 na kupewa jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi wote wanaoishi visiwani humo.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, alisema lengo la kuwapo kwa mkutano huo ni kufanya majadiliano ya pamoja kati ya watendaji wa wizara ya afya, washirika wa maendeleo na wadau ili kupata njia mbadala za kitaalamu zitakazowezesha serikali kugharamia huduma za matibabu kwa wananchi.

Hafidh alisema gharama za huduma ya matibabu zimekuwa zikipanda siku hadi siku, jambo linalosababisha wananchi wengi kutomudu kuchangia pale inapobidi, hivyo Serikali ya Zanzibar imeona ipo haja ya kukaa pamoja na wadau wa maendeleo ili kutafuta namna bora itakayosaidia kupunguza changamoto hizo.

# Wanaojenga maeneo ya hifadhi kukiona

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini imesema haitomvumilia mtu yeyote anayejenga katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya uchimbaji visima vya maji safi na salama.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Joseph Kilangi, aliyasema hayo wakati akikagua eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa visima vya maji huko Maungani, Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Alisema serikali imeshafanya tathmini ya maeneo hayo lakini jambo la kushangaza ni wamikili wake kuwauzia viwanja wananchi wengine kinyume na utaratibu.

Alisema kwa mujibu wa sheria eneo likishafanyiwa tathmini linakuwa mali ya serikali na halifai kutumika kwa shughuli yoyote ya kijamii.

"Eneo hili tayari limeshafanyiwa tathmini na waliyokuwa wamiliki wake baadhi ya fedha tushawalipa, sasa inakuwaje wanauza viwanja," alihoji Katibu Kilangi.

Alisema wizara haiwezi kuwavumilia watu hao kwa vile wanafanya mambo kinyume na utaratibu wa sheria, hivyo aliwataka viongozi wa wilaya na mkoa kuwachukulia hatua ili iwe fundisho kwa wengine.

Katibu Kilangi alisema uamuzi wa wizara kwa sasa ni kuwawekea alama za X ili kubomoa nyumba zao na kupisha ujenzi wa visima vya maji safi na salama vitakavyotatua changamoto ya upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi.

"Kwa sasa uamuzi ni kuendelea kusitisha ujenzi katika maeneo hayo na kuwaomba vyombo vinavyohusika kufanya majukumu yao,"alisema.

Alisema wizara hiyo haina lengo la kuwanyanyasa wananchi bali jambo la msingi ni kufuata sheria zilioko ili maendeleo na malengo ya serikali yafikiwe. Aliwakumbusha wananchi kuwa makini pindi wanapotaka kununua maeneo, kuzingatia matakwa ya kisheria ili kuepuka migogoro kwa wananchi na taasisi nyingine.

Sheha wa Shehia ya Maungani, Khamis Bonzo, alisema watu wengi katika maeneo hayo wanapojenga au kununua viwanja hawawashirikishi masheha na badala yake huuziana kienyeji.

Alisema hapo awali walikuwa wanawasimamisha wananchi wanaokuta wanajenga katika maeneo hayo, lakini wanazidiwa na baadhi ya madalali ndiyo maana umetokea uvamizi huo. Baadhi ya wananchi waliyouziwa katika maeneo hayo akiwamo Suleiman Ali Muhammed alisema hawakujua kuwa maeneo hayo hayaruhusiwi kujengwa ndiyo maana wakatoa fedha na kununua viwanja.

Alisema wananchi wengi walionunua viwanja katika maeneo hayo hawana utamaduni wa kuwashirikisha watu wa ardhi wala masheha kwasababu huona wanapoteza muda.



**MARIOO**
UKURASA 12





# MZEE KING KIKII AMETUACHIA MENGI
## Rais Samia amtaja kama mwalimu

WATANZANIA wamegubikwa na huzuni baada ya mwanamuziki nguli wa Dansi Nchini, Boniface Kikumbi Mwanza Mpango maarufu kama King Kikii, kuaga dunia jana.

Kutokana na msiba huo mzito kwa wapenzi wa muziki wa dansi, Rais Samia Suluhu Hassan, ametoa salamu za rambirambi kwa Watanzania, familia na marafiki akiwataka kuwa na moyo wa uvumilivu katika kipindi hicho kigumu.

King Kikii ambaye wimbo wake 'Kitambaa Cheupe' umekuwa maarufu kwa miongo kadhaa sasa, amefariki Dunia nyumbani kwake akiwa na miaka 77.

Mtoto wake Joseph Kikumbi, alithibitisha kuwa baba yake amefariki jana majira ya saa 7:30 usiku baada ya kuzidiwa akiwa nyumbani kwake Mtoni kwa Aziz Ally Wilaya ya Temeke.

"Mzee alikuwa akisumbuliwa na maradhi mbalimbali, wiki mbili zilizopita alikuwa Muhimbili tuliomba ruhusa tumrudishe nyumbani kutokana na hali yake na mpaka anafariki alikuwa akiugua tezi dume na saratani ya ini."

Shughuli za mazishi zinafanyika nyumbani kwake, na wanatarajia kumpumzisha katika makaburi ya Kinondoni baada ya taratibu kukamilika.

Wakati wa uhai wake, Mzee King Kikii alikuwa kinara katika bendi mbalimbali ikiwemo Fouvete, Marquis Original, Orchestra Safari Sound (OSS) maarufu kama wana Ndekule, Orchestra King Kikii Double O, Orchestra Sambulumaa Band, Zaita Musica na Capitale Wazee Sugu.

Katika salamu zake za rambirambi, Rais Samia amesema Kwa zaidi ya miaka 50 King Kikii ametoa burudani kwa mamilioni ya Watanzania, na amekuwa mlezi na mwalimu wa wengi katika tasnia ya muziki.

"Tutamkumbuka na kumuenzi kwa kazi zake nyingi na nzuri ikiwemo wimbo wake maarufu wa 'Kitambaa Cheupe' ambao umeendelea kuwa sehemu ya burudani kwenye maeneo na shughuli mbalimbali za burudani nchini" amesema Rais Samia.

BASI SAWA

## Ndaro hataki umbea



MSANII wa uchekeshaji, Ndaro, amewatetea wasanii wanaonunua magari ya kifahari, akisema ni wakati wao kujiongezea thamani.

Amesema kuna wakati ukifika msanii anatakiwa kuna baadhi ya vitu hapaswi kuhusika navyo ikiwamo kupanda magari ya dadala au kutumia bodaboda.

"Gari linaongeza thamani ya msanii, ukifika mahali unapofikia huwezi kupanda daladala au kutumia bodaboda kila mtu atakushangaa," amesema Ndaro.

## Godson ya Marioo hiyooo



MWANAMUZIKI nyota, Marioo, amewapa presha mashabiki wake ambao kila kukicha wanahesabu siku ili kuiona Albam yake mpya aliyoiita GodSon.

Albam hiyo itakuwa album ya pili baada ya 2022 kutoa THE KID YOU KNOW ambayo imefanya vizuri katika majukwaa ya muziki na kutajwa ilikuwa bora kwa wasanii wa Bongo Fleva nchini.

Kulingana uongozi wa msanii huyo, albamu hiyo itakuwa na nyimbo zinazotamba ikiwamo I miss You, Anisamehe, Siwezi, Dear Ex, Mi Amore na My Life




## SHAMSA KAWAPA USHAURI WAKE

MWIGIZAJI mkongwe wa Bongo Muvi, Shamsa Ford, amewashauri wanawake kuacha tabia ya kuomba huruma kwa watu wengine, badala yake waende kufanya kazi ili kujikomboa.

Amesema hakuna binadamu aliyeumbwa akiwa hana thamani, kwani nguvu na bidii inasababisha kupata kipato kinachoweza kukupatia upendo.

"Acha kujitiisha huruma na kumuambia kila mtu shida zako binadamu wa sasa hivi ukiwa huna kitu huthaminiki wanathaminiwa wenye pesa toka nje nenda kapambane na maisha," amesema Shamsa.





## Tatoo za Harmonize zaibua mjadala

MSANII maarufu wa Bongo Fleva, Harmonize, ameibua mjadala baada ya kuonekana mwili wake wote ukiwa umetapakaa tatoo.

Hivi karibuni, Harmonize aliweka video katika ukurasa wake wa Instagram, akiwa hana shati na kuonyesha jinsi mwili wake ilivyochorwa tattoo zenye taswira mbalimbali.

Baadhi ya watu walioangalia video hiyo walitoa maoni tofauti, huku wengi wakionekana kutokubaliana na michoro iliyojaa katika mwili wa msanii huyo wakieleza haina maana kimaadili ya Kiafrika.

## WAKIKUSUTA WANAKUSUUZA

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE filamu za Kibongo kuna wasanii wa aina tofauti na vipaji mbalimbali. Si kila msanii ana kipaji cha kuigiza sehemu ile ile, ingawa inapaswa msanii kuwa na uwezo wa kuigiza sehemu zote unazopangiwa.

Lakini kila msanii ana umahiri wa aina yake na wa kipekee kuigiza sehemu fulani kiasi cha hata watazamaji kudhani ndiyo tabia yake halisi.

Baadhi ya wasanii wa kike wanaigiza kama kinadada au kinamama ambao wana maneno ya shombo, nyodo na kuwa na tabia ya kwenda wao wenyewe au kukodiwa kwenda kuwazodoa au kuwasuta wenzao kwa sababu mbalimbali zinazohusu maisha ya uswazi.

Lakini sifa ya mtu huyo ni lazima awe na mineno ya shombo.

Kwenye filamu za Kibongo ikishafika sehemu kama hiyo ya kuzodoana, kusutana wapo wasanii wenye uwezo mkubwa wa kazi hiyo.

### Riyama Ally

Ni msanii wa kike mwenye kipaji cha hali ya juu ya uigizaji. Ana uwezo wa kuigiza sehemu nyingi zinazotal...a. Lakini kwa miaka ya hivi karibuni ameonekana kuwa ni mahir. sana kuigiza sehemu za kuzodoana, kusutana kutokana na kuwa na maneno mengi ya shombo, kejeli, nyodo, mizaha, akizipangilia kwenye nahau, misemo, methali na kila aina ya neno ambalo ataona litamuudhi au kumkera mgomvi wake.

### Chuma Suleinam 'Bi Hindu'

Siyo kama alikuwa anaigiza tu. Ni kweli alikuwa na uwezo mkubwa ya kuongea. Ni mama aliyejaaliwa maneno mengi, hasa ya Kipwani, kutokana na kuwa ni mzaliwa na jiji la Dar es Salaam. Sina haja ya kumueleza sana kwani watazamaji wa filamu wanalifahamu timbili lake. Ukimchokoza huyu ujue umelikoroga. Hutopigwa makofi, lakini maneno yake yanaweza kukufanya uwe kama umepigwa. Alifariki dunia 2022 jiji Dar es Salaam.

### Tausi Mdegela

Awali alionekana kama msanii wa kawaida tu, lakini kadri siku zilivyozidi kusonga mbele ameonekana kuwa ni mmoja kati ya wasanii wenye uwezo mkubwa ya kuongea kwa kuwapa makavu laivu wenzake kwenye filamu.

Mbishi na mwenye uwezo mkubwa wa kuzungumza na maneno ya shombo juu. Huyu ni Tausi Mdegela, msanii mwenye muonekano wa kipekee, lakini pia ni kipenzi cha watoto mitaani.



### Asha Boko

Ni maarufu sana kwenye filamu za ucheshi. Ni mwoga wa kupigwa, lakini mdomoni yuko vizuri.

Ni mmoja wa waigizaji mwenye uwezo wa hali ya juu wa kike nchini na hasa zile za kusemana, kucharurana na kusutana.

### Shamsa Ford

Ni mmoja wa wasanii maarufu wa kike nchini Tanzania mwenye uwezo mkubwa wa kuigiza. Lakini hakuna aliyejua kuwa naye ana uwezo wa kuigiza kama mwanadada wa uswahilini. Filamu chache alizoigiza mambo ya swazi, zimesababisha wengi kugundua kipaji chake kingine cha kuweza kuongea na kuwa na tabia zile zile za huko.

FILAMU

# Mission Town, Mjini shule

**Na Adam Fungamwango**

HII filamu inaitwa 'Mission Town'. Ina mambo mengi ya kuangalia na kujifunza. Tutaangalia jinsi madawa ya kulevya yanavyokuwa janga kubwa kwenye dunia ya sasa. Tunaona jinsi baadhi ya askari polisi waliopewa dhamana ya kulinda raia na mali zao, pamoja na kuzua uhalifu, wanapokuwa moja ya hao wahalifu.

Lakini pia jinsi mtu anavyoweza kufanya lolote lile, hata kwa kukiuka taaluma yake kwa ajili ya kuilinda familia yake. Tunajifunza jinsi baadhi ya watu tunaowaamini, lakini wao ndiyo wanaweza kukuangaliza. Pia tutaona jinsi watu wema wenye nia nzuri na jamii na taifa letu kwa ujumla wanapogeuka wao kuwa kama hawalifu na hatari ya kupoteza maisha inakuwa juu yao.

Imechezwa na wasanii Kassim Mkoka, Almasi Said, Grace Mapunda, Lucky Lukamo, Omari Lyombe, Emari Daudi na wengineo.

Mr. Matty ni mkuu wa genge na kuingiza na kusambaza madawa ya kulevya nchini ambaye ana mtandao hadi kwa baadhi ya maaskari na maafisa ya polisi, hivyo hakamatiki.

Askari mmoja anadhulumiwa mgao wake na kuamua kutoa siri kwa mwandishi wa habari Feruzi. Mwandishi huyo anaamua kulianika genge hilo kwenye gazeti. Hapo ndipo taflrani inapoanza.

Mr. Matty analituma genge lake kumtafuta mwandishi huyo. Wanachofanya ni kumteka mke wa mhariri wa gazeti. Mhariri Marko anapigiwa simu ofisini kuambiwa mkewe ametekwa na wanachotaka ni jina la mwandishi wa habari aliyeandika habari hiyo. Pamoja na kwamba hatakiwi kufanya hivyo, lakini aliwapa ili mkewe aachiwe.

Faruzi anakamatwa, lakini bado watekaji waliendelea kumshikilia Maria mke wa mhariri.

Kama vile haitoshi, wanamteka pia mhariri, pamoja na mpenzi wa mwandishi Feruzi.


Kitu ambacho walikuwa hawakijui ni kwamba mpenzi wa mwandishi Tunda ana uwezo mkubwa kwenye sanaa ya mapigano. Anafanikiwa kutoka. Anakwenda nyumbani kwa mhariri na kukutana na kijana wake Emari ambaye pia baba na mama yake wametekwa. Emari pia ni mzuri kwenye sanaa za mapigano.

Wanaamua kuungana na kuanza kulisambaratisha kundi lote la Mr.Matty kwa ajili ya kuwaokoa wapendwa wao. Emari baba na mama yake, Tunda mpenzi wake Feruzi.

Wanafanikiwa kuliteketeza kwa umahiri wa upiganaji na kuwafanya askari polisi waaminifu kuwa na kazi ndogo tu ya kwenda kumkamata mkuu wa genge hilo Mr. Matty, huku Emari na Tunda wakifanikiwa kuwaokoa wapendwa wao.



# Ivy hapendi ugomvi



MKE wa mwanamuziki wa Nigeris, Paul Okoye, amesema anachukizwa na ugomvi unaoendelea kati ya mumewe na pacha wake Peter Okoye.

Ivy Zenny, kupitia video iliyosambaa mitandaoni amesema amesema hawezi kuishi kwa raha huku akiwaona ndugu hao mapacha wakikosa maelewano kama familia moja.

Akijibu maswali ya mashabiki wake, Ivy amesema kamwe hawezi kuwa na tabia ya kutomwamini mume wake na kufariji, licha ya yanayoendelea katika familia yao.



## Skai kupata mtoto wa kwanza

MWIGIZAJI nyota wa filamu za zamani za Disney Channel, Skai Jackson (22), amethibitisha kuwa ana ujauzito wa mtoto wake wa kwanza.

Msanii huyo alionekana akitembea kando ya mitaa ya Los Angeles akiwa amevalia suruali ya jeans na fulana nyeupe, huku akiwa tumbo lake likiwa limeongezeka kiasia.

Mwigizaji huyo alilithibitishia jarida la People kuwa baba wa mtoto wake ambaye hajazaliwa ni mpenzi wake, ambaye bado hajamweka hadharani.


## Gilmore awasuta wanaomdhihaki

TAYARISHAJI wa maudhui ya mitandao ya kijamii nchini Nigeria, Gilmore, amesema ni makosa kwa kutilia shaka utajiri aliopata kutokana na kazi hiyo.

Akizungumza hivi karibuni, amefafanua kwamba sio vizuri kuweka dhana potofu kwa kila kitu wanachofanya watu wenye fani hiyo, kwa sababu wanatumia muda mwingi kuweka sawa maisha yao.

Amesema kazi hiyo inaweza kumudu kupata vitu vya kifahari kama vile magari na nyumba, kwa sababu kila tone la usingizi linafanyiwa kazi.





## Enioluwa awatetea waigizaji

MSANII wa filamu kutoka Nollywood, Enioluwa, ameibuka na kuelezea sababu ambazo zinafanya tasnia ya filamu nchini huko kuwatumia wasanii waliozoeleka.

Akijibu swali la mtumiaji mmoja wa mtandao wa X ambaye alisema kuchoshwa na kuona filamu nyingi zinawahusisha wasanii walewale, Enioluwa amesema tayarishaji wengi wanataka kazi zao ziwe na ufanisi na ndio maana wanachagua wasanii wanaojitambua.

"Mara nyingi watu wanasema wamechoka kuona sura zilezile kwenye filamu za Nigeria. Hata hivyo, tofauti na Hollywood, waigizaji wa Nigeria hawana uwezo wa kufanya filamu moja tu kwa mwaka,tasnia kwa sasa haiwezi kusaidia wageni wengi kama watu wanavyotarajia kwa sababu, kiuhalisia, wengi wao hawawezi kukidhi hata mahitaji yao," amesema.

## Wengi watamfuata P Diddy

WAKILI ambaye anawatetea watu 120 walioathiriwa na vitendo vya unyanyasaji dhidi ya rapa maarufu wa Marekani, P Diddy, amesema watu wengine mashuhuri watahusishwa katika mashtaka hayo.

Wakili Tony Buzbee, ameuambia mtandao wa TTMZ, kwamba watu hao wakiwemo wasanii, wanasiasa na wafanyabiashara maarufu waliohudhuria kwenye pati zilizoandaliwa na Diddy, hata kama hawakufanya chochote, watatakiwa kujibu kutokana na kutazama kwao bila kuchukua hatua.

Buzbee amesema ikiwa kulikuwa na watu kwenye matukio ya ajabu ambao walitazama watu ambao walidhulumiwa kingono baada ya kunyweshwa dawa na hawakufanya lolote kukomesha, kisheria wana hatia.

Ameongeza kuwa tayari ameandika barua akiomba mahakama kuwaita baadhi yao.





# Waziri apongeza TANAPA ukusanyaji mapato

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, amepongeza menejimenti na watumishi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) kwa kazi nzuri ya uhifadhi na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Alitoa pongezi hizo jana jijini hapa alipotembelea makao makuu ya TANAPA katika ziara yake ya kikazi. "Mkakati wa kulinda maliasili ukiwa ndani ya eneo lako ndio haswa ninaoutaka na ninyi TANAPA mnatekeleza vizuri, hili unapokuwa ndani ni rahisi kuwasoma majangili natoa maelekezo kwa taasisi zote chini ya wizara kuja kujifunza TANAPA na kwenda kulitekeleza hili," alisema Balozi Chana.

Pia aliziagiza taasisi zote za wizara kuzingatia maelekezo ya mawaziri nane, kuhusu utatuzi wa migogoro ya mipaka, 4R za Rais Samia Suluhu Hassan na kusisitiza uadilifu kwa askari na watendaji wote na kubainisha kuwa ni jukumu kubwa la kuhifadhi ambalo walilopewa kwa niaba ya watanzania.

Kamishna wa Uhifadhi-TANAPA, Musa Nassoro Kuji, alifafanua mafanikio mbalimbali ya shirika hilo ikiwemo juhudi zinazofanywa na TANAPA, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali pamoja na wanyamapori, uboreshaji wa huduma za utalii, utekelezaji wa mfumo wa Jeshi la Uhifadhi pamoja na ukusanyaji wa mapato.

"Kwa miaka minne hadi Septemba mwaka huu, hakukuwa na tukio lolote la kuuawa kwa faru kutokana na ujangili, pia matukio ya ujangili wa Tembo yamepungua kutoka 15 mwaka 2016/2017 kufikia matukio matatu katika mwaka 2023/2024,"alisema.

Aidha, Kamishna Kuji alipongeza Serikali, kwa kuruhusu upanuzi wa Hifadhi ya Taifa Serengeti kujumuisha eneo la Ghuba ya Speke na kulipa fidia zao wananchi walio katika kaya 3,885 sawa na asilimia 91 na tayari wameshaanza zoezi la kuhama kupisha shughuli za uhifadhi katika eneo hilo.



Ofisa Ushirika Mwandamizi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Ndimolwo Laizer (kushoto), akizungumza wakati akiwajengea uwezo viongozi na jamii wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, kuhusu kujiunga na ushirika, katika kikao kilichofanyika Mji mdogo wa Orkesumet, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mtandao waandaa tuzo kwa wanahabari

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MTANDAO wa Vikundi vya Wakulima na Wafugaji Mkoa wa Arusha (MVIWAARUSHA) kwa kushirikiana na washirika wa mradi wa KEA (IDP,CARI) wameandaa tuzo za wandishi wa habari wa masuala ya mfumo endelevu wa chakula na kilimo Ikolojia mwaka huu.

Akizungumza jana jijini hapa, Katibu wa Kamati ya Tuzo hizo, Imani Hazron, alisema lengo la kutoa tuzo hizo ni kutambua na kusherehekea uandishi wa habari uliotukuka kwenye masuala ya kilimo endelevu, usalama wa chakula na uendelevubwa mifumo ya chakula.

Alisema pia tuzo hizo zinalenga kuhamasisha ubora katika uandishi wa habari,kuhimiza ufuatiliaji wa kina kuhusu mbinu za kilimo cha kiikolojia na kuongeza uelewa wa umma kuhusu umuhimu wa mifumo endelevu ya chakula mbele ya changamoto za mabadiliko ya tabianchi na ongezeko la idadi ya watu.

"Waandishi wa Habari watakaoshiriki tuzo hii, ni wale ambao wamefundishwa na kushiriki katika kazi mbalimbali za mradi wa kilimo endelevu," alisema. Aidha, alisema fomu za ushiriki wa tuzo hizo, zitatolewa kwenye mitandao na kwenye website yao ya https:/www.mviwaarusha.or.tz

Alisema kazi zinazostahili kupelekwa kwa ajili ya ushindani lazima ziwe zimefanyika kuanzia mwaka 2022 hadi Novemba 10 mwaka 2024 na hiyo kutokana na mafunzo yalitolewa na kuanzia hapo walishirikiana na waandishi kufanya shughuli mbalimbali za usalama wa chakula na mifumo endelevu ya chakula na kilimo Ikolojia.

Ezron alisema uwasilishwaji wa kazi utakuwa wa wiki mbili kuanzia Novemba 13 hadi Novemba 28 mwaka huu.

Alisema kwenye mashindano hayo kutakuwa na tuzo lakini pia kutakuwa na zawadi nono ya fedha kwa kiasi kilichopangwa kama motisha ya kuendelea kufanya jitihada za kuelemisha na kuhabarisha zaidi jamii.

# DC ataka uwazi utoaji wa mikopo

**Na Jaliwason Jasson,**
BABATI

MKUU wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Emmanuela Kaganda, amesema mchakato wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa makundi maalumu uwe wazi na shirikishi kwa wananchi wenye sifa na hatarajii kupokea malalamiko juu ya fedha hizo anahitaji haki itendeke kwa kila mtu.

Kaganda alitoa agizo hilo jana wakati akitoa maelekezo ya serikali katika Baraza la madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Babati.

"Mchakato wa utoaji wa mikopo uwe wazi na shirikishi ili mwenye sifa aweze kushiriki, sitarajii kupokea malalamiko juu ya hizi fedha," alisema Kaganda.

Aidha alisema dosari zilizokuwepo lisijirudie na kusiwepo uonevu kupendeleana kwa kuwa kila Mwananchi mwenye sifa ana haki kupata mkopo ilimradi ana sifa.

"Watakaopata wawe kweli wanastahili kupata mikopo na madiwani tukahamasishe siyo ndugu zetu ni wale wahitaji,"alisema.

Katika hatua nyingine mkuu huyo wa wilaya amewaagiza viongozi kuanzia ngazi ya chini mpaka wilaya watatue migogoro ya ardhi na siyo kuwa sehemu ya kuhamasisha migogoro ya ardhi mpaka kusababisha wataalamu washindwe kufanya kazi.

Kaganda alisema pale atakapokuta migogoro ya ardhi atasimama na sheria na kanuni katika kutatua migogoro hataangalia cheo cha mtu.

Alisema kuna sehemu zingine wataalamu wanashindwa kufanya kazi wanaenda wanashikiwa mapanga hivyo hawawezi kuwa na utawala ndani ya utawala.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Babati Shaaban Mpendu alisema zaidi ya sh. Mil. 500 ndizo zimetengwa ila zilishatolewa sh. Mil. 211 na fedha wanazodai kwa watu waliokopeshwa ni sh. Mil.80 ambapo deni hilo ni himilivu.

Pia diwani wa viti maalum Zainab Sige aliomba madiwani kupewa miongozo ya mikopo ili waweze kutoa elimu kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Abdulaaman Kololi, alisema maelekezo yote ya serikali wameyapokea na watayafanyia kazi.

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# ‘Kubwa la Maadui’ mzee Ashanti

**Na Adam Fungamwango**

UNAPOZUNGUZIA filamu za Kihindi kama hujamzungumzia mzee Amrish Puri, basi utakuwa hujakamilisha utamu wa picha hizo ambazo kwa watoto, vijana na wazee wa miaka ya mwanzoni mwa 1980 hadi mwanzoni wa miaka ya 1990 walikuwa wakizitazama sana kwenye kumbi mbalimbali za sinema kama Drive In, New Chox, Empire, Avalon na sehemu nyingine.

Alijulikana sana kwa majina mbalimbali ya kibabe, wengine wakimwita ‘bandidu’, na kule Arusha walimfahamu kwa jina la ‘Nyambisi’, lakini India na sehemu zungine duniani wanamfahamu kwa jina la ‘Mogambo’.

Jina aliitwa kutokana na kulitumia kwenye moja kati ya picha nyingi ambazo amecheza.

Dar es Salaam na mikoa mingine nchini Tanzania, alijulikana kama mzee Ashanti. Hili ndilo jina maarufu zaidi nchini na wakati mwingine ukitaja jina lingine, wengine wanakuwa hawamfahamu ni nani.

Jina la Ashanti alilipata kutokana na filamu moja aliyoicheza mwaka 1882, ilitwayo ‘Ashanti’.

Unyama alioufanya humo, watoto wa wakati huo waliamua kumpa jina la mzee Ashanti, na hata akionekana kwenye filamu nyingine na hata akitumua jina lingine, lakini wao wakimuona tu basi utasikia ‘adui kwenye picha hili ni mzee Ashanti’.

Wengine wakamwita jina la ‘Kubwa la Maadui.”

Umaarufu wa mzee huyu ni kucheza kama adui kwenye filamu zake zote alizocheza wakati wa uhai wake, zaidi ya asailimia 90.

Filamu ambayo akicheza kama mtu wa kawaida tu mwenye roho nzuri, mpenda watu, mwenye hekima na busara, watu wanakuwa hawaipendi. Ni kama wanaiona haina uhalisia.

Mzee Ashanti akicheza kama adui, kila anayeiangalia atataka atazame ubabe wake, ukatili wa kiwango cha juu, mwenye uwezo wa kumtesa na kumuua yoyote yule ambayo atahatarisha mamlaka yake, utajiri wake, au kitu chochote ambacho yeye anaamini yuko sahihi.

Hucheza kama mtu muonevu, asiye na ubinadamu, mpenda makuu, katili, mvunja sheria, huku akiwaweka mfukoni baadhi ya maafisa wa polisi, na hata majaji wasio waaminifu.

Kutokana na kucheza kwa uhalisia mkubwa, alikuwa akipata mikataba mingi ya kucheza filamu nyingi tofauti.

Na hii inatokana na mashabiki wengi wa filamu za Kihindi kupenda kumuona na kupata uhalisia wa ukatili wa mzee huyo dhidi ya wananchi na mastelingi ambao mara nyingi hupata tabu naye tabu mno, kabla ya kupata ushindi dakika za mwisho.

Ndiyo maana amecheza na wababe wote maarufu wa filamu za Kihindi kama kina Amitabh Bachchan, Sunny Deol na wengineo. Sidhani kama hajacheza na staa yoyote unayemfahamu wa miaka ya 1980 hadi 1990.

Inavyoonyesha soko la filamu la Kihindi lilitambua kuwa ili filamu ipendwe na kuuzwa sana, ni lazima mzee Ashanti awepo.

Tafuta stelingi yoyote yule, lakini kwenye nafasi ya adui lazima awepo mzee huyo ili mambo yaende

Hizi ndizo moja ya shughuli zake kwenye filamu, kiasi cha kuwaliza baadhi ya watazamaji kwenye roho ndogo, hasa akinadada na akinamama wanapokuwa akiangalia. Yaani hana shoo ndogo.

Shabiki mmoja wa filamu za Kihindo aliniambia kuwa alikuwa anamchukia kwa dhati kabisa mzee huyo kutokana na udhalimu wake, licha ya kwamba anafahamu kuwa alikuwa akiyafanya mbele ya kamera tu.

Habari kutoka nchini India zinasema kuwa nje ya filamu, mzee huyo alikuwa mtu wa watu sana na amesaidia watu wengi, ikiwemo masikini nchini India.

Alizaliwa Juni 22, 1932 na alifariki dunia Januari 12, 2005 nchini India kwa ugonjwa wa kansa.

Ataendelea kukumbukwa kizazi kwa kizazi, si nchini India tu, bali duniani kote kwa mashabiki wa filamu za Kihindi kuwa ndiye adui katili zaidi kuwahi kutokea kwenye filamu hizo mpaka sasa.

**Tuma meseji 0716 350534**





HABARI KIMATAIFA

# Iran yakubali kupitiwa mpango wa nyuklia

**TEHRAN,** IRAN

IRAN imesema iko tayari kutatua masuala yenye utata kuhusu mpango wake wa nyuklia kabla ya Donald Trump hajaingia madarakani Januari mwakani.

Rais wa Iran Masoud Pezeshkian, alimueleza Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Nishati ya Atomiki (IAEA) Rafael Grossi, kwamba serikali yake iko tayari kutatua masuala yenye utata kuhusu mpango huo.

Grossi ambaye alikuwa na ziara nchini humo, alisema kwamba mazungumzo hayo yalikuwa na tija kuhusu nyuklia ya Iran.

Alisema taarifa hiyo ni muhimu ili kuepusha mzozo mpya katika eneo la Mashariki ya Kati ambalo tayari limegubikwa na vita vya Israel dhidi ya Hamas na Hezbollah.

Aidha, Grossi alitahadharisha kwamba mitambo ya nyuklia ya Iran haipaswi kushambuliwa.

Ziara yake inafanyika siku chache baada ya waziri mpya wa ulinzi wa Israel, Israel Katz kusema Iran iko hatarini zaidi kuliko hapo awali.

Pezeshkian alimwambia Grossi kwamba mara nyingi nchi yake imethibitisha nia yao njema ya utayari wa kushirikiana na kuungana na shirika hilo la kimataifa kutatua utata unaodaiwa kuwepo na mashaka juu ya shughuli ya amani ya nyuklia inayofanywa na nchi hiyo.

Kuna wasiwasi kwamba Trump ambaye ana msimamo mkali dhidi ya Iran, huenda akaipatia Israel nafasi huru ya kuishambulia baada ya kuchukua madaraka mwezi Januari.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Abbas Araghchi, ambaye pia alikutana na Grossi, alisema Iran ilikuwa tayari kufanya mazungumzo kwa kuzingatia maslahi ya kitaifa na haki zisizoweza kuepukika.

Araghchi alikuwa mpatanishi mkuu wa Iran katika mazungumzo ambayo yalipelekea makubaliano ya kihistoria ya nyuklia ya 2015 na mataifa makubwa, ambayo Trump alijiondoa miaka mitatu baadaye.

Grossi pia alikutana na mkuu wa shirika la nishati ya atomiki la Iran, Mohammad Eslami.

Eslami aliuambia mkutano wa pamoja wa waandishi wa habari kwamba Iran itachukua hatua mara moja dhidi ya vikwazo vyovyote kutoka kwa bodi ya IAEA.

"Azimio lolote la uingiliaji kati katika masuala ya nyuklia ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran bila shaka litakabiliwa na hatua mara moja," alisema Eslami.

Ziara ya Grossi ni ya pili mjini nchini Iran kwa mwaka huu.

**DW**



Kikosi cha zimamoto nchini Syria kikipambana na moto uliosababishwa na shambulizi la Israel katika jiji la Damascus jana. **PICHA: REUTERS**

# HRW: Israel imefanya uhalifu wa kivita Gaza

**NEWYORK,** MAREKANI

SHIRIKA la haki za binadamu Duniani la Human Right Watch (HRW) limesema Israel imefanya uhalifu wa kivita na uhalifu dhidi ya ubinadamu kwa kuwahamisha kwa makusudi Wapalestina kwenye makazi yao katika Ukanda wa Gaza.

Katika ripoti yake, limesema watu milioni 1.9, sawa na asilimia 90 ya wakazi wa Gaza, wamekimbia makazi yao katika kipindi cha mwaka uliopita.

Limeeleza asilimia 79 ya eneo hilo liko chini ya maagizo yaliyotolewa na Israeli.

Ripoti hiyo ya HRW ilisema hatua hiyo ni sawa na uhamisho wa lazima na kwamba ushahidi unaonesha kuwa umekuwa ni utaratibu na sehemu ya sera ya serikali.

Pia ilisema vitendo vya Israeli vinaonekana kukidhi kuangamiza kizazi cha kikabila".

Hata hivyo, Israel ilisema ripoti hiyo ni ya uongo na imejitenga na ukweli.

"Kinyume na madai katika ripoti ya HRW, juhudi za Israel zinaelekezwa tu katika kusambaratisha uwezo wa ugaidi wa Hamas na sio kwa watu wa Gaza," alisema Oren Marmorstein, msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Israel katika chapisho lake kwenye mtandao wa X.

Aliongeza kuwa Israel itaendelea kufanya kazi kwa mujibu wa sheria ya migogoro.

HRW pia imeshutumu Hamas kwa kutumia raia kama ngao kwa kufanya kazi ndani ya nyumba na miundombinu ya kiraia. Wakati huo huo, Shirika la habari la serikali ya Syria linasema kuwa watu 15 wameuawa wakati wa mashambulizi ya anga ya Israel kwenye majengo mawili ya makazi watu magharibi mwa jiji la Damascus.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, moja ya majengo yaliyoshambuliwa yapo katika kitongoji cha Meze mjini Damascus, ambayo ni makao makuu ya taasisi za usalama, balozi na mashirika ya Umoja wa Mataifa.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, jengo la pili liko katika kitongoji cha Qudsiya magharibi mwa Damascus.

Shirika la Habari la Uingereza (Reuters) iliandika kwamba Israeli, ilithibitisha mashambulio hayo kwa kueleza kwamba yaliyoshambuliwa ni maeneo ya jeshi pamoja na makao makuu ya Islamic Jihad.

Kwa mujibu wa shirika la habari la Associated Press, Ofisa wa kundi la Palestina Islamic Jihad nchini Syria, ambaye hakutaka jina lake litajwe, ameliambia shirika hilo moja ya ofisi zake ililengwa katika shambuliohilo.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, anayemaliza muda wake Joseph Borrell, ametaka kusitishwa kwa majadiliano ya kisiasa na Israel kuhusu wasiwasi wa maswala ya haki za binadamu katika Ukanda wa Gaza.

Borrell anatarajiwa kuwasilisha pendekezo hilo wakati wa mkutano wa mawaziri wa mambo ya nje wa Umoja wa Ulaya utakaofanyika nchini Ubelgiji hivi karibuni.

Mmoja wa wanadiplomasia aliyeshiriki katika mazungumzo hayo, alisema mkuu huyo wa sera za kigeni ameziandikia nchi wanachama kuziomba zisitishe mazungumzo hayo kati ya Umoja wa Ulaya na Israel.

Msemaji wa Tume ya Ulaya Peter Stan, alisema Borrell, atawataka mawaziri waangalie iwapo Israel inakiuka haki za binadamu, inaheshimu au haiheshimu sheria za kimataifa juu ya haki za binadamu kwa mujibu wa vifungu husika kwenye Makubaliano ya Muungano.

Kwa sasa Umoja wa Ulaya umegawanyika kuhusu vita kati ya Israel na Wapalestina na kuna uwezekano mkubwa kwamba mawaziri hao watapinga pendekezo hilo.

**BBC**

# JANGA LA KUPOROMOKA KWA HADHI NA THAMANI YA BABA

**Na Dk. Enock Mlyuka**



WANADAMU kwa sasa wanaishi katika jamii inayobadilika kwa kasi kutokana na maendeleo ya sayansi, teknolojia ya habari na mawasiliano ya habari. Mwingiliano wa watu, utamaduni na itikadi umekuwa mkubwa na rahisi.

Pamoja na mazuri mengi, maendeleo haya yamekuja na changamoto nyingi. Miobngoni mwa changamoto hizo ni kuongezeka kwa uovu duniani, mmomonyoko wa maadili, ubinafsi, kushamiri kwa migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi.

Aidha, mashauri ni mengi kuhusu kinababa wasiowajibika na wanaokwepa majukumu ya familia. Hali hii imesababisha taasisi ya familia kuwa katika mgogoro na hadhi ya 'baba' imeanza kuporomoka katika jamii ya leo.

Kumeshuhudiwa jitihada nyingi za kuwawezesha mabinti ambazo haziendi sambamba na uwezeshaji wa vijana wa kiume. Vijana wengi wa kiume wa leo hawafunzwi na kuandaliwa kuwa wanaume na baba watendaji, walezi, wapambanaji katika maisha na viongozi wa familia.

Hali hii inachangia kuwapo kwa vijana wengi tegemezi, wasiowajibika na wenye kutaka kulelewa au maisha ya mteremko. Kwa kusisitiza hoja hii, mama mmoja alisema, Vijana wengi wa leo wamekuwa madume ya mbegu ya kuzaa tu na sio kutunza na kulea.

Changamoto hii ambayo inaweza kuitwa kuwa ni janga la taifa, inaweza kuendelea kuwa kubwa katika jamii kama vijana wa kiume hawatafunzwa na kuandaliwa ipasavyo kuwa wanaume, viongozi na baba bora kuanzia ngazi ya familia. Jukumu hili linawahusu kinababa zaidi kuliko kinamama.

Faukwa ya hayo, magonjwa yasiyo ya kuambukiza yameongezeka katika jamii. Wataalamu wa afya wanabainisha kwamba msongo wa mawazo unachochea na kusababisha magonjwa yasiyoambukiza kama vile maradhi ya moyo, changamoto ya afya ya akili, kisukari, shinikizo la damu, saratani na kiharusi.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) takribani watu milioni 350 duniani wameathiriwa na magonjwa yasiyoambukiza ambayo chanzo chake ni msongo wa mawazo. Inaelezwa na wataalamu wa afya kwamba msongo wa mawazo wa muda mrefu kwa sehemu kubwa unachangia matatizo ya kiafya na vifo vya kinababa wengi.

Baba ni msingi na kioo cha familia. Kwa upande mmoja, baba akisimama vizuri kwenye nafasi yake ya kuwa baba, atakuwa chanzo cha baraka, furaha, mafanikio na ustawi wa familia. Kwa upande mwingine, baba asiposimama vizuri kwenye nafasi yake ya kuwa baba anaweza kuwa chanzo cha laana na mateso katika familia.

Tangu kuumbwa kwa ulimwengu, Mwenyezi Mungu alikusudia baba awe chimbuko la uzao, nguvu kazi, furaha, baraka na ustawi. Wajibu huu unahitaji nidhamu, utii kwa Mwenyezi Mungu na kujituma.

Nini asili ya neno 'baba'? Neno 'baba' limetokana na neno la Kiebrania 'Ab', ambalo katika lugha ya Kiaramu (Aramaic) ni 'Abba'. Neno 'Ab/Abba' maana yake ni chanzo (source), mwendelezaji (sustainer), mtunzaji (nourisher) na mlinzi (protector). Kwa lugha ya Kigiriki neno 'Pater' limetumika. Kwa ujumla, 'baba' ni zaidi ya kuzaa. Kwa hiyo, kinachomfanya mwanamume aitwe 'baba' ni majukumu aliyoyabeba kwa ajili ya familia yake.

**Kabla ya kutungwa na kuwepo kwa mifumo rasmi ya kisheria, baba alitambulika kama:**

- **Mkuu wa Familia**
  Baba alikuwa anachukuliwa kama kichwa cha familia, mwenye mamlaka na wajibu wa kufanya maamuzi muhimu kwa niaba ya familia. ndiye aliyesimamia mali na rasilimali za familia, na kuhakikisha kuwa kila mwanafamilia anapata mahitaji ya msingi kama vile chakula, mavazi, na malazi.

- **Mlinzi na Mlezi**
  Baba alikuwa na jukumu la kuhakikisha usalama wa familia yake dhidi ya hatari za nje, kama vile wanyama wakali, majirani wabaya, au makundi ya maadui. Aidha, alikuwa na jukumu la kuwafundisha watoto wake stadi za maisha, mila na desturi za jamii, na maadili mema.

- **Mfumo wa Urithi**
  Katika jamii nyingi za zamani, baba alikuwa na jukumu la kurithisha mali na jina la familia kwa watoto wake wa kiume. Hii ilikuwa na maana ya kudumisha nasaba na kuendelea kwa ukoo.

- **Mwalimu wa Maadili na Mila**
  Katika familia nyingi za ki-Afrika, baba alikuwa na jukumu la kuweka misingi ya nidhamu. Baba alikuwa kiongozi wa kiroho na kiutamaduni katika familia, akiwafundisha watoto wake desturi, mila, imani ya dini na jamii. Alikuwa mhusika mkuu katika sherehe na matukio muhimu kama vile tohara, harusi, na sherehe za kuvunja ungo. Misingi ya nidhamu na familia kwa ujumla iliwekwa na baba na kulelewa na mama. Watoto waliwaheshimu sana baba zao, lakini waliwatukuza sana mama zao.

- **Mchumi wa Familia**
  Baba alikuwa mtafutaji mkuu wa riziki kwa familia yake. Katika jamii za kilimo, baba alikuwa akilima na kuhakikisha mavuno yanapatikana. Katika jamii za wawindaji, baba alikuwa anawinda na kukusanya chakula kwa ajili ya familia.

- **Mfano wa Kuigwa**
  Baba alionekana kama mfano wa kuigwa na watoto wake, hasa wa kiume, ambao walitarajiwa kumfuata katika matendo na maamuzi yake. Hii ilikuwa muhimu katika kudumisha utamaduni na mfumo wa kijamii.

- **Msimamizi wa Ndoa na Uhusiano**
  Baba alikuwa na jukumu la kusimamia ndoa na masuala ya uhusiano ndani ya familia, akihakikisha kuwa watoto wake wanapata wachumba sahihi na kuwaandaa kwa maisha ya ndoa.

- **Kiungo cha Watoto na Ukoo**
  Baba alikuwa kiungo cha watoto na ukoo. Hii ndio sababu ya watoto katika jamii nyingi za ki-Afrika kuchukua jina la ukoo la baba. Mtoto hakuwa wa baba na mama pekee, bali wa ukoo na jamii pia. Mtoto alilindwa na kuweza kuadibishwa na jamii pia.

Kwa ujumla, kabla ya sheria za kisasa, baba alikuwa na jukumu la msingi katika kudumisha familia na jamii. Nafasi yake ilijumuisha uongozi, ulinzi, matunzo, urithi, maadili, uchumi, mambo ya kiroho na usimamizi wa ndoa na uhusiano.

Majukumu haya yalitambulika na kukubalika kijamii, na kuendelezwa kupitia tamaduni na desturi za jamii husika. Hata hivyo, hali ilivyo katika jamii ya leo inauweka mustakabali wa 'baba' njia panda.

Katika nyakati hizi za maendeleo na mabadiliko ya kijamii, baba anapaswa kuwa rafiki zaidi wa watoto wake kuliko kuogopwa ili watoto wawe huru kumweleza hisia, mawazo, matamanio na changamoto zao. Baba hapaswi kupanda mbegu ya uharibifu kwa watoto wake.

Ni jukumu la baba kuwafunza na kuwaandaa watoto wake wa kiume kuwa wanaume na baba bora wenye kuwajibika. Haya yatawezekana kama baba atakuwa na muda wa kutosha na watoto wake na mawasiliano mazuri.

Hali hii hujenga uhusiano mwema kati ya baba na watoto wake. Kwa kufanya hivyo, baba huwahakikishia watoto wake kuwa yeye ni muhimu katika maisha yao.

Ni dhahiri kwamba jinsi baba anavyokuwako katika maisha ya watoto wake leo, ndivyo watoto wake watakavyokuwa katika maisha ya baba yao hapo baadaye. Kwa hiyo, baba akisimama vizuri kwenye nafasi yake ya kuwa baba itamwongezea heshima na thamani katika familia na jamii kwa ujumla.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-39

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**




Sisi wenyewe madaktari baada ya uchunguzi wa pili tukaanza kuulizana, ilikuwaje ikawa hivyo?

Ndiyo tukapata taarifa za uhakika kuwa waliomuua ndiyo waliotumia pesa ili kupindisha uchunguzi wa kwanza. Na hao hao walitaka kushinikiza uchunguzi wa pili uwe kama wa kwanza, tukakataa. Tukautoa kama ilivyo. Tukapata taarifa sasa kuwa wale wale jamaa, wamekwenda kutoa pesa kwa baadhi ya askari polisi wasio waaminifu wamsingizie mtu mwingine kesi ya mauaji baada ya taarifa sahihi kutoka na kuwaridhisha ndugu na wananchi. Nilishangaa na kupatwa na simanzi niliposikia eti 'aliyepewa kesi ya kichwa', ni mchumba wake. Kwa maana hiyo binafsi niliingiwa na huruma sana. Ndiyo maana alipojitambulisha nikamuahidi kuwa nitamsaidia kwa hali na mali hadi ukweli ujulikane," Dokta Shija bado aliendelea kutoa ushahidi mahakamani.

Akasema kutokana na hilo alikwenda kumshirikisha mdogo wake ambaye ni askari polisi aliyekuwa ndiyo kwanza anaanza kazi kama miezi sita tu iliyopita kuhusu jambo hilo.

"Kwa sababu nilimwambia mtu huyu mimi nataka kumsaidia na yeye akasema atatumia taaluma yake ya upolisi ili kumsaidia ingawa kwa kificho kwa sababu hatari Jeshi la Polisi limeshamuweka kuwa mtuhumiwa, hivyo alifanya kazi kwa kificho ili kusaka ukweli bila kuwashirikisha waajiri wake, hadi walipombaini bosi wa Kamal ndiyo anahusika, jinsi walivyofanya nadhani shadihi wa nne, mdogo wangu Willy Shija atakuja kuelezea zaidi."

Shahidi mwingine alikuwa na afande Willy. Alikiri kusimuliwa kisa hicho na kaka yake dokta Shija.

"Mimi niliona kwenye televisheni na kusoma kwenye gazeti juu ya mkasa huu. Ripoti ya kwanza na ya pili zote nilizisoma. Kwa sababu kaka yangu ni daktari alikuja kuniambia kuwa kuna utata na hata huyu mchumba wa Mariamu inawezekana kuwa siyo muuaji. Siku chache baadaye akaja kuniambia kuwa amekutana na kijana anayetafuta na Jeshi la Polisi akidaiwa kuwa muuaji wa mchumba wake. Akaniambia baada ya maelezo kama alivyofikiria, si kweli kama muuaji. Akamsimulia jinsi ilivyotokea.

Kaka akaniomba tumsaidie kijana yule. Mimi nikamwambia ni kosa kufanya kazi ambayo sijatumwa na mwajiri wangu. Akaniambia ni sawa, lakini akasema hata huko kuna watu ambao si waaminifu. Inawezekana wakubwa wameambiwa mambo ambayo siyo. Wapo wanaokula rushwa ambao wanashirikiana na wahalifu, ndiyo maana wamepindisha mpaka ripoti ya mauaji kwa kuwapa rushwa hata madaktari. Akaniambia kwa upande mmoja inaweza ikawa ni kosa, lakini kwa upande wa pili unaweza ukawa shujaa wa taifa. Nikaona ni bora nisaidie, lakini kwa kificho, ndiyo nikakutana na mhusika, tukaongea nikaanza uchunguzi wangu na yeye nikishirikisha," alisema afande Willy.

**"Nilipa kazi afande mmoja kuchukua ufunguo mmoja wa jengo ambalo moja Makumbusho zilipo ofisi za Materu, akatoa kopi na kutengeneza ufunguo wa bandia, ambao ulitusaidia kuingia kwa hila kwenye jengo la ofisi hizo pamoja na kuchukua ushahidi.**

Afande aliendelea kuwa alianza kuchukua namba za watu waliotumia meseji za viztisho Kamal na wale waliomtumia meseji za mapenzi marehemu Mariamu.

"Namba zilionekana zimesajiliwa maeneo ya Tabata kwa majina tofauti na nilimpa kazi mwenyewe Kamal kwenda kufuatilia na tulipata majina ya watu ambao walisajili tukaambiwa walikuja siku moja.

Niliwakamata mimi mwenyewe na wote wakaniambia walitumwa na Boniphace Materu. Nilimwita Kamal abaye alikuwa hajui lolote na kumuuliza kama anamfahamu mtu huyu. Alishtuka na kuniambia kuwa ni bosi wake.

Kila mmoja anamfahamu Materu kuwa ni mmoja na wafanyabiashara wakubwa nchini, lakini kujua kama anaweza kuhusika na hili ilikuwa haiaminiki.

Akaniambia ni bosi wake, kwa sababu ni mmiliki wa gereji kubwa pale Buruguni ambayo yeye ni kama msimamizi wake.

Nikamwambia basi huyu ndiye anayeonekana kuwatuma watu watatu kusajili namba ambazo ndizo zilitumika kutuma meseji kwa Mariamu, na pia kwako kukutisha.

Waheshimiwa kwa sababu nina maaskari ambao ni rafiki zangu walianza kunisaidia kumpeleleza bila kujua na kugundua mambo mengi machafu, ikiwemo kuwa na vikao vya siri ambavyo vilirekodiwa na flashi zilikuwa zikitunzwa kwenye mmoja ya droo zilizopo ofisini kwake," Afande Willy alizidi kutoa ushahidi.

"Nilipa kazi afande mmoja kuchukua ufunguo mmoja wa jengo ambalo moja Makumbusho zilipo ofisi za Materu, akatoa kopi na kutengeneza ufunguo wa bandia, ambao ulitusaidia kuingia kwa hila kwenye jengo la ofisi hizo pamoja na kuchukua ushahidi.

Kazi tuliyoifanya baada ya hapo ni kuanza kufanya uchunguzi ni, magazeti, redio na televisheni gani zinaweza kutumika kuanzisha sakata hilo.

Tulichokuja kubaini ni kwamba tayari Materu na wapambe wake walikuwa wameshapita kwenye vyombo vingi vya habari na kujaribu kuzuia habari yoyote itakayomhusu.

Alifanikiwa kwa kiasi fulani, lakini baadhi ya waandishi za uchunguzi walipata fununu ya hilo wakatutafuta kuisaka habari hiyo.

Waandishi watatu wa magazeti walikutana sisi eneo la siri ambalo hata wao hawakujua ni wapi, wakamhoji Kamal kuhusu kuhusika kwake kwa mauaji ya mpenzi wake, ndipo alipowahadhithia kila kitu ikiwemo ushahidi unaoonyesha kuwa bosi yake, Materu ndiye aliyehusika kwa mauaji hayo.

Akawapa ushahidi wa maandishi na video ili hata kama akishtaki, basi ajikaange mwenyewe kwenye mafuta yake.

Siku tatu baadaye, kwa msaada wa kama dokta Shija, waandishi wengine wa habari za mitandao ya kijamii walipelekwa eneo lingine kwa ajili ya mahojiano.

Nao waliambiwa kila kitu, na kupewa ushahidi, ambao wanahabari zote walikuwa wakipewa kopi, hata flashi nazo zikipopiwa na kupestiwa, ili mwenyewe abaki na ushahidi halisi ambao ungeweza kumsaidia kuepuka kesi inayomkabili.

Baada ya kukamilisha zoezi hilo, ndipo habari zikaanza kurushwa, kitu ambacho kikabadilisha kila kitu. Kilibadilisha mtazamo wa raia na askari polisi juu ya mauaji ya mrembo Mariamu. Materu alikamatwa na kuletwa hapa. nadhani kwangu huu ndiyo mwisho wa ushahidi, vielelezo vyote tumevikabidhi, tunaiachia mahakama tukufu," alimaliza afande Willy kutoa ushahidi wake ambao ulikuwa ni wa mwisho upande wa mashtaka. Kilichobaki sasa ilikuwa ni kupangwa tarehe kwa ajili ya siku ya washtakiwa kujitetea.

Itaendelea Jumamosi

# KALLY AAHIDI KUINYANYUA KMC NA KUTUPA 'DONGO'

**Na Faustine Feliciane**

KOCHA Mkuu mpya wa KMC FC, Kally Ongala, amesema atapambana kuhakikisha anaitoa timu hiyo ilipo katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kuiweka nafasi salama.

KMC inashika nafasi saba katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 14 kibindoni baada ya kucheza michezo 10 huku vinara wa ligi hiyo wakiwa ni Simba yenye pointi 25 wakifuatiwa na Yanga yenye pointi 24.

Kally amejiunga rasmi na timu hiyo ya Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam juzi ikiwa ni siku chache baada ya aliyekuwa Kocha Mkuu, Abdihamid Moallin, kutangaza kuondoka ndani ya klabu hiyo.

Tetesi zinasema huenda Moallin akajiunga na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga kama Kocha Msaidizi huku bado ‚upepo' ukiwa haujatulia kwa Kocha Mkuu, Miguel Gamondi.

Akizungumza jijini jana, Kally, alisema anafahamu changamoto na ushindani uliopo katika ligi hiyo lakini atajitahidi kuhakikisha anakiimarisha kikosi chake ili kucheza mpira wa kiwango cha juu.

Kally alisema katika hakuna mechi rahisi na amejipanga kuwaimarisha na kuwajenga wachezaji wake kwa kutohofia wapinzani.

"Nitajaribu kuwa mkweli katika dunia ya uongo, nitapambana sana kuhakikisha KMC inasogea kutoka hapa ilipo, nitakuwa mkweli kwenye kila kitu, nawashukuru KMC kwa nafasi waliyonipa," alisema Kally.

Kocha huyo alisema ushirikiano wa pamoja kati yake, wachezaji, viongozi na mashabiki utaisaidia timu hiyo kufanya vyema na kufikia malengo.

"Nafahamu ligi ni ngumu sana, kila timu inapambana kutafuta ushindi, lazima tushirikiane pamoja ili kuipa makali KMC," Kally aliongeza.

Mechi ya kwanza ya kocha huyo mpya itachezwa Novemba 24, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma dhidi ya wenyeji Dodoma Jiji.

# KMKM yajipanga kuimaliza KVZ FC

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KMKM SC inatarajia kuvaana na Maafande wenzao wa KVZ FC katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa kwenye Uwanja Mau A visiwani hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema jana wamejiandaa vyema kuhakikisha wanapata ushindi ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo.

Msimu alisema wanataka kupunguza tofauti ya pointi na timu zilizoko juu katika msimamo na hatimaye kufikia malengo ya kuwania taji la ubingwa.

Kocha huyo alisema mchezo huo ni muhimu kwa upande wao baada ya kutokuwa na mwendelezo mzuri katika michezo iliyopitaya.

"Tumejiimarisha na tunaenda kupambana kusaka ushindi, tunajua hatukuwa na matokeo mazuri katika michezo yetu miwili iliyopita, tumefungwa mara mbili mfululizo," Msimu alisema.

Aliongeza anajua mchezo huo hautakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wanaokutana nao pia wana mipango na malengo ya kuondoka na pointi tatu.

„Wapinzani wetu watakuja na mbinu ya kutafuta ushindi, ili kuhakikisha tunafanikiwa kuchukua alama tatu lazima tuingie na mpango kazi jambo ambalo KMKM pia mpango wao upo hivyo hivyo," kocha huyo alisema.

Aliongeza katika kuhakikisha mbinu zao za kusaka ushindi zinafanikiwa, tayari wamekifanyia maboresho kikosi chao katika nafasi ya viungo ambayo ilionyesha mapungufu kwenye michezo iliyopita.

"Tumejiandaa kuwakabili wapinzani wetu kivyovyote lakini tunahitaji kupata alama tatu, tunataka kukamilisha mzunguko huu wa kwanza tukiwa kwenye nafasi nne za juu, ili tufikie malengo yetu, ni lazima michezo hii iliyobaki tupate ushindi," aliongeza.

KMKM inashuka dimbani ikiwa na pointi 16 mkononi baada ya kushinda michezo minne, sare michezo minne na wamefungwa michezo miwili wakati wapinzani wao, KVZ wapo nafasi ya tano baada ya kujikusanyia pointi 17.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 15 wakifanya mazoezi ili kujiandaa na mashindano ya shule ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika hivi karibuni nchini Uganda. **PICHA: TFF**

# Mafunzo yapaa kileleni Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MAAFANDE wa Mafunzo wametinga kileleni baada ya kuifunga JKU SC bao 1-0 katika mechi ya raundi ya 11 Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau B juzi jioni.

Ushindi huo umeifanya Mafunzo kufikisha pointi 23 huku nafasi ya pili ikikaliwa na Mwembe Makumbi City yenye pointi 22 na inafuatiwa na Mlandege yenye pointi 21 baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 na Uhamiaji.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Mafunzo, Abdallah Bakari, alisema licha ya kupata ushindi huo mwembamba alikiri mchezo ulikuwa mgumu.

Kocha huyo alisema kila timu ilitinga uwanjani ikicheza kwa kujihami na kujilinda ili kuzuia mashambulizi ya upande wa pili.

**"Tumefanikiwa lengo la kupata ushindi katika mchezo huu, pongezi ziende kwa wachezaji wangu walifanya kazi kubwa sana, mchezo ulikuwa mgumu, lakini walijitu ma sana, " alisema kocha huyo.**

Aliongeza wanarudi katika uwanja wa mazoezi kujiandaa na mchezo unaofuata dhidi ya Mwembe Makumbi City utakaofanyika Novemba 25, mwaka huu.

Bingwa wa Ligi Kuu Zanzibar atapata nafasi ya kukiwakilisha kisiwa hicho katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMTAKA KUDUS

KLABU ya Arsenal iko tayari kutumia pauni milioni 83 kumnunua kiungo wa kati wa West Ham, Mohammed Kudus, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ghana mwenye umri wa miaka 24 akitaka kujiunga na Washikabunduki hao ili kucheza mashindano ya Ulaya. ***(Fichajes)***

### SPURS YAMBANIA ROMERO

TOTTENHAM Hotspur iko tayari kukataa nia mpya ya Real Madrid ya kumnunua beki wa Argentina, Cristian Romero, mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

### ZIRKZEE AGEUKA LULU

KLABU ya Manchester United inafikiria kumtoa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Joshua Zirkzee, mwenye umri wa miaka 23 Januari huku timu mbalimbali zinazoshiriki Ligi ya Serie A zikimfuatilia. ***(Calciomercato)***

### DAVID ATAKIWA JUVE

KLABU ya Juventus iko mstari wa mbele katika mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Canada, Jonathan David, mwenye umri wa miaka 24, kutoka Lille huku Manchester United, Liverpool na Inter Milan pia zikimwania nyota huyo. ***(Footmercato)***

### MAIGNAN ANUKIA CITY

MANCHESTER City imeelekeza macho yake kwa mlindamlango wa AC Milan na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Mike Maignan, mwenye umri wa miaka 29.***(Mail)***

### BELLINGHHAM SOKONI

MABOSI wa Borussia Dortmund wanafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Sunderland mwenye umri wa miaka 19, Jobe Bellingham, katika dirisha dogo la Januari. ***(Alan Nixon via Newcastle Chronicle)***

### DAVIES AICHAGUA BARCA

BEKI wa Bayern Munich, Alphonso Davies, yuko tayari kuungana tena na kocha wake wa zamani, Hansi Flick, katika klabu ya Barcelona licha ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada mwenye umri wa miaka 24 kutakiwa Real Madrid na Manchester United. ***(Team Talks)***

### POGBA, JUVE KUMALIZANA

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba, mwenye umri wa miaka 31, anakaribia kufikia makubaliano ya kusitisha mkataba wake na Juventus na kusaini na klabu nyingine kama mchezaji huru pindi muda wake wa kufungiwa utakapokamilika. ***(Sky Sports)***

### SANE, BAYERN KUTETA

WINGA wa Ujerumani, Leroy Sane, ameonyesha nia ya kusaini mkataba mpya na Bayern Munich, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 bado hajafikia makubaliano kuhusu mkataba huo na klabu hiyo. ***(Florian Plettenberg)***

### TAH ATAJWA MADRID

MLINZI wa zamani wa Hispania, Sergio Ramos, mwenye umri wa miaka 38, hatarejea Real Madrid lakini watasajili beki wa kati ifikapo Januari, huku beki wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Jonathan Tah (28), akikaribia kutua klabuni hapo. ***(Diario AS)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BARCELONA : HATUNA MPANGO NA HAALAND

## ●●● Klabu hiyo yasema kwa sasa Lewandowski anawapa furaha na…

**BARCELONA, Hispania**

MKURUGENZI wa Michezo wa Barcelona, Deco, amedai klabu hiyo kwa sasa haitazamii kusajili mshambuliaji mpya kama Erling Haaland au Viktor Gyokeres kwa sababu wanafurahishwa na huduma ya Robert Lewandowski, imeelezwa.

Lewandowski amefunga mabao mengi zaidi ya mchezaji yeyote katika ligi tano bora za Ulaya kufikia sasa msimu huu akiwa na magoli 14 ya LaLiga kufikia sasa, pia akifunga mara tano kwenye Ligi ya Mabingwa. Haaland amefunga mabao mawili pungufu katika mchezo wa ligi na amehusishwa kama nyongeza ya safu ya mbele ya Barca katika siku zijazo.

Huku Lewandowski akitarajiwa kufikisha umri wa miaka 37 ifikapo Agosti, mwakani Barca watahitaji kuleta mchezaji mpya.

Hata hivyo Deco amedai hatua hiyo bado haijafikiwa.

Aliiambia Mundo Deportivo: "Kwanza tunapaswa kujua kama Haaland ndiyo tunamtaka kwa siku zijazo. Hatujui hilo sasa.

„Kwa sasa hatutaki yoyote. Tunaye Robert. Hatujapanga chochote na kipaumbele kwa sababu tunapaswa kuzingatia msimu huu.

"Gyokeres ni mchezaji mzuri, amekuwa akifunga mabao kwa muda huko Ureno, tunamfahamu kama tunavyowafahamu wengine, lakini sio kipaumbele kwetu kwa sasa.

"Wakati ukifika wa kufanya uamuzi na lazima nifanye kwa sababu tutazingatia chaguzi. Lakini sidhani kama ni wakati mwafaka wa kuzungumza juu ya mchezaji yeyote.

"Nadhani ni vigumu sana kupata mshambuliaji kama Robert siku hizi. Kuna mmoja au wawili wa kiwango hiki. Labda Haaland au mwingine. Hakuna wengi wa kiwango hiki wanaopatikana.

"Lakini hatutakata tamaa ya kutafuta mshambuliaji yeyote kwa sasa kwa sababu tutazingatia kwanza kile Robert anaweza kufanya. Hakika nadhani anafuraha kuwa hapa. Ni mshindi na kama tutakuwa na msimu mkubwa mimi nadhani atataka kubaki.

"Tunamtaka Robert aendelee kuwa na furaha, kufunga mabao na kusalia angalau msimu mmoja zaidi."

HABARI MICHEZO

## Salah, Liverpool hakijaeleweka

**LIVERPOOL, England**

MAZUNGUMZO juu ya mkataba mpya kati ya Liverpool na Mohamed Salah yanaendelea, lakini bado yako mbali kufikia mwafaka, kwa mujibu ripoti.

Salah ni mmoja wa wachezaji watatu wa Liverpool ambao wanatazamiwa kuwa huru msimu ujao wa joto.

Nyota wengine ni Virgil van Dijk na Trent Alexander-Arnold, hali ya kimkataba ya mshambuliaji huyo wa Misri imetawala mazungumzo yanayoizunguka Liverpool - ingawa wachezaji wanaonekana kutoshtuka.

Kikosi cha Arne Slot kiko kileleni katika jedwali la Ligi Kuu England na Salah anasisitiza klabu hiyo inaweza “kushinda mataji yote” ikiwa atasalia Merseyside baada ya mwisho wa Juni, 2025.

Wakati timu ya usimamizi ya Salah bado inajadili kwa dhati madai na matarajio mbalimbali ya mteja wao juu ya mkataba wake mpya, Sky Sports ya Ujerumani inaripoti hakuna makubaliano ambayo yamefikiwa.

Salah alikua mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi katika historia ya Liverpool alipoongeza mkataba wa miaka mitatu katika msimu wa joto mwaka, 2022.

Licha ya kuingia msimu wa mwisho, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 anabakia kuwa winga bora zaidi wa kulia duniani.




## Vidic ashauri wachezaji wavivu United wauzwe

**MADRID, Hispania**

MLINZI wa zamani wa Manchester United, Nemanja Vidic, amekosoa vikali wachezaji wa sasa wa klabu hiyo, akihoji “tabia” zao na kutaka baadhi yao kuuzwa katika dirisha lijalo la usajili.

Beki huyo wa kati wa Serbia alitumia muda wa miaka nane na nusu kuitumikia klabu hiyo ya Old Trafford akifanya kazi chini ya Kocha Sir Alex Ferguson.


Erik ten Hag alikuwa kocha wa tano wa kudumu wa klabu baada ya Ferguson na alifanikiwa kushinda mataji mawili kabla ya kutimuliwa Oktoba, mwishoni mwaka huu.


“Sote tunatarajia zaidi kutoka kwao,” alisema Vidic akiiambia Sky Sports wakati wa mapumziko ya kimataifa ya Novemba hii.

“Hata sasa tuna wachezaji wa ajabu,” bingwa huyo mara tano wa Ligi Kuu England alikiri, kabla ya kuongeza: “Nadhani swali langu ni zaidi kuhusu wahusika, uimara, kuwa tayari kushindana, kutoa ziada na kushindana wiki baada ya wiki.

“Nakumbuka nilipokuwa nikiichezea Man United. Chris Smalling, Phil Jones, Jonny Evans, nilikuwa nikifikiria wote wanakuja kuchukua nafasi yangu. Niliogopa ningepoteza nafasi yangu. Na hiyo ni kawaida na nilijituma. Hakuna mtu aliyelazimika kuniambia hivyo.

“Kwa hiyo kazi inahitaji kufanywa katika madirisha machache yajayo ya uhamisho. Sio tu wachezaji ambao watawaleta, nadhani baadhi ya wachezaji lazima wajaribu kutafuta timu mpya.”





# KANE AKERWA NYOTA KUIKACHA ENGLAND

**LONDON, England**

NAHODHA wa England, Harry Kane, ameonyesha kukerwa na idadi ya wachezaji wa kikosi hicho wanaoondoka kwa visingizio mbalimbali ikiwamo majeraha akiamini kuchezea timu ya taifa ni fahari zaidi ya kitu chochote kile.

Kwa mujibu wa Daily Mail, Kane, hafurahishi na wachezaji kudai wana majeraha na kujiondoa kambini.

“Nadhani kuitumikia England ni jambo bora zaidi, ni bora kuliko kitu chochote. England ni bora kuliko klabu ni jambo la muhimu sana kufanya kama mchezaji,” alisema Kane.

Aliongeza, “Sio jambo la busara kuikacha timu ya faifa, lazima tuwe wazalendo.”

Kauli hiyo ya Kane imekuja wakati huu ambao wachezaji tisa wa timu hiyo wameondoka kikosini kwa sababu mbalimbali.

Wachezaji hao ni Aaron Ramsdale, Trent Alexander-Arnold, Levi Colwill, Declan Rice, Bukayo Saka, Cole Palmer, Jack Grealish, Phil Foden na Jarrad Branthwaite akikamilisha orodha hiyo hapo jana.

# PAMBA JIJI FC YAITISHA SIMBA IKIWAZA REKODI

**Na Adam Fungamwango**

HUKU ikiendelea kujiimarisha, Pamba Jiji FC imewataka Simba ya Dar es Salaam kutotarajia mteremko katika mechi itakayowakutanisha ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Novemba 22, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Mathias Wandiba, amesema Simba anakwenda Mwanza katika wakati mbaya kwa sababu malengo yao ni kushinda mechi nne zilizobaki za mzunguko wa kwanza.

Wandiba alisema Pamba Jiji inawaambia Simba wajiandae kukutana na ushindani kutokana na wao kuhitaji ushindi katika mechi zote zilizobakia za mzunguko wa kwanza ambazo watacheza nyumbani.

"Dhamira yetu ni kufanya vizuri katika michezo yetu minne iliyobaki ya mzunguko wa kwanza, michezo miwili tutacheza nyumbani dhidi ya Simba, Ijumaa ijayo na KenGold, Desemba Mosi, hii tumejiwekea mikakati ni lazima tushinde, kwa bahati nzuri moja kati ya michezo hii mwili tunacheza na Simba, wamekuja kwenye wakati mbaya.

Unapocheza na timu kama Simba ni lazima wachezaji wawe vizuri kichwani kiakili, huwezi tu kusema tunatumia mfumo huu, sijui nini, ni lazima uwaweke wachezaji wako vizuri kisaikolojia, kwa sababu wanaweza wakaingia wakafanya kitu hicho kikawaondoa kwenye mchezo moja kwa moja," alisema kocha huyo.

Aliongeza anaamini katika mchezo huo Pamba Jiji inaweza kupata ushindi wa kwanza nyumbani kutokana na maandalizi na maboresho ambayo wamefanya ndani ya kikosi chao.

Pamba Jiji imeshinda mechi moja tu msimu huu ambapo ilikuwa ugenini dhidi ya Fountain Gate, ikiwafunga mabao 3-1, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa mkoani, Manyara.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Pamba Jiji iko kwenye nafasi ya 15, ikiwa na pointi nane, baada ya michezo 11, ikishinda mmoja, sare tano na kupoteza michezo mitano.



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya walemavu kutoka sehemu mbalimbali wakifanya mazoezi ili kujiimarisha kwenye Uwanja wa JMK Park jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Coastal kuchaguana Desemba 16

**Na Somoe Ng'itu**

KLABU ya Coastal Union inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajia kufanya uchaguzi mkuu ifikapo Desemba 16, mwaka huu, imeelezwa.

Uchaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa katiba ya klabu hiyo baada ya viongozi waliokuwepo kumaliza muda wa kukaa madarakani miaka minne.

Taarifa rasmi iliyotolewa na Katibu wa Kamati ya Uchaguzi ya klabu hiyo, Linda Lugano, ilisema mchakato wa kuchukua fomu kwa wagombea ulianza jana kwa wadau mbalimbali kusisitizwa kujitokeza kwuania nafasi za uongozi.

"Napenda kuweka wazi mwisho wa kuchukua fomu ni Jumatatu ya Novemba 18, mwaka huu saa 9:00 mchana, fomu zinapatikana katika ofisi ya klabu ya Coastal Union FC," alisema katibu huyo.

Lugano alitaja nafasi zitakazowaniwa katika uchaguzi huo ni pamoja na mwenyekiti, makamu mwenyekiti, wajumbe wawili wa Kamati ya Utendaji ya klabu hiyo.

Alisema gaharama ya kuchukua fomu ya kuwania uenyekiti ni Sh. milioni moja, makamu ni Sh. 500,000 na wanaotaka kugombea ujumbe wa kamati ya utendaji watalipia fomu kwa sh. 200,000.

Wanachama wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wanafanya uchaguzi ili kujiandaa na uchaguzi wa shirikisho hilo utakaofanyika mwakani.

## Gamondi yametimia, apigwa faini

INATOKA UK. 24

kutimuliwa kwa kocha huyo kufuatia kupoteza mechi mbili mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara hivi karibuni.

Yanga iliruhusu kufungwa na Azam FC bao 1-0, mechi iliyochezwa Novemba 2, mwaka huu na siku tano baadaye ikachapwa na Tabora United mabao 3-1, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Mbali na vipigo hivyo, taarifa zilisema kocha huyo amekuwa akiwaamini baadhi ya wachezaji, huku wengine akishindwa kuwapa nafasi ya kuonesha uwezo wao.

Hata hivyo, Gamondi, aliitengeneza Yanga imara iliyokuwa ikicheza soka la kasi, bila kutegemea mchezaji mmoja kama awali ilipokuwa ikimtegemea zaidi mshambuliaji, Fiston Mayele.

Gamondi ambaye ameweka rekodi ya kuifikisha Yanga katika fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, alitua Yanga kuchukua mikoba ya Nasreddine Nabi, ambaye kwa sasa anaifundisha Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini.

Yanga imemtangaza rasmi Mjerumani Sead Ramovic kuchukua mikoba ya Gamondi.

Taarifa zaidi zinasema, tayari uongozi wa Yanga umempa mkataba wa miaka miwili, Abdihamid Moallin, ambaye mapema wiki hii alitangaza kujiuzulu nafasi yake ndani ya klabu ya KMC kuwa Kocha Msaidizi.

Pia Mjerumani Sead Ramovic, naye anahusishwa na mchakato wa kutua Jangwani.

Wakati huo huo, Gamondi amekumbana na balaa jingine baada ya kufungiwa michezo mitatu na kupigwa faini ya Sh. milioni mbili kwa kosa la kumsukuma na kumwangusha chini kocha wa viungo wa Singida Black Stars, Sliman Marloene, baada ya kutokea mabishano baina yao, kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar, timu hizo zilipokutana Oktoba 30, mwaka huu.

Kamati hiyo pia imefuta adhabu ya kadi ya njano aliyoonyeshwa beki wa Yanga, Ibrahim Hamad ‚Bacca', katika mechi dhidi ya Coastal Union iliyochezwa Oktoba 26, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

Kamati imesema imejidhihirisha kutokana na marejeo ya picha mjongeo na taarifa za wataalam kuwa Bacca hakustahili adhabu hiyo.

## Morocco: Tunataka ushindi tu leo Stars

INATOKA UK. 24

Mkapa, Dar es Salaam, timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana.

Stars yenye pointi nne ipo katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa kundi hilo nyuma ya Guinea yenye pointi sita huku Ethiopia inaburuza mkia kiwa na pointi moja.

Mechi nyingine ya kundi hilo itachezwa leo kati ya Guinea dhidi ya DR Congo ambayo tayari ina pointi 12 kibindoni.

# Michezo

Jumamosi Novemba 16, 2024

Nipashe


**Barcelona : Hatuna mpango na Haaland**

UKURASA 21





# Gamondi yametimia, apigwa faini

Kocha mpya ni Mjerumani Sead Ramovic...



Gamondi

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

HATIMAYE yametimia, uongozi wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ya jijini, Dar es Salaam umetangaza rasmi kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu yao, ambaye ni raia wa Argentina, Miguel Gamondi, imethibitishwa.

Hadi kufikia jana, Gamondi, alikuwa amekiongoza kikosi cha Yanga kwa muda wa msimu mmoja na nusu.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo inasema wameamua kuvunja mkataba bila kutaja sababu yoyote huku ikiongeza mchakato wa kusaka kocha mpya umeshaanza haraka.

"Uongozi wa Yanga unapenda kuutaarifu umma umevunja mkataba na Kocha Mkuu wa kikosi cha kwanza, Gamondi (Angel Miguel).

Vile vile, uongozi umesitisha mkataba wa kocha msaidizi wa kikosi hicho, Moussa Ndaw, klabu inapenda kuwashukuru na kuwatakia kila la heri katika majukumu yao mapya.

Tayari mchakato wa haraka wa kutafuta kocha mpya wa kikosi chetu unatarajiwa kukamilika hivi punde," ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Taarifa hiyo inakamilisha tetesi za

INAENDELEA UK. 23

Mshambuliaji wa Taifa Stars, Simon Msuva, akijiandaa kupiga mpira katika mazoezi ya timu hiyo itakayokutana na Ethiopia katika mechi ya Kundi H ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), itakayochezwa leo Mjini Kinshasa, nchini DR Congo. **PICHA: TFF**

## Morocco: Tunataka ushindi tu leo Stars

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kukutana na wenyeji Ethiopia katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Des Martyrs, Kinshasa nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo).

Mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania na Ethiopia imeamua kucheza mechi zake Kinshasa kwa sababu ya kutokuwa na viwanja venye hadhi ya kutumiwa katika michuano inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Stars inahitaji pointi tatu muhimu leo na pia kuifunga Guinea katika mechi ya mwisho ya Kundi H itakayofanyika Novemba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco', amesema ameshawaandaa vijana wake kwa ajili ya kusaka ushindi.

"Maandalizi yameshakamilika, nimejaribu kuwaelekeza vijana wangu nini cha kufanya na kupunguza madhaifu yote yaliyoonekana katika michezo iliyotangulia, niseme tuko vizuri na lengo letu ni kupata pointi tatu ambazo zitatusogeza kwenye mlango wa kuingilia kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON)," alisema kocha huyo.

Nahodha wa Stars, Mbwana Samatta, aliliambia gazeti hili yeye na wachezaji wenzake wote wanaelewa umuhimu wa mchezo wa leo, hivyo watajitoa kupambana ili kupata ushindi kwa sababu endapo watashinda katika mchezo huo watajiweka kwenye wakati mzuri zaidi.

"Kila mchezaji anafahamu umuhimu wa mchezo huu na unaofuata, sidhani kama kuna muda wa kukumbushana tena.

Mwalimu ameshamaliza kazi yake, ametupa mbinu na mipango, ni jukumu letu sasa kuonesha uwanjani. DR Congo wameshafuzu, tunagombea nafasi moja, sisi (Tanzania) na Guinea ndiyo tunapewa nafasi kubwa, hivyo tunataka tuitumie nafasi hiyo," alisema Samatta.

Katika mchezo wa mzunguko wa kwanza uliochezwa Septemba 4, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Benjamin

INAENDELEA UK. 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002